
SUPA JACKPOT
TZS.1,029,401,974
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Saratani ya kinywa janga lingine nchini**

UKURASA 3



**Tuchel atimuliwa Chelsea**

UKURASA 21


# Nipashe

Alhamisi Septemba 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581062

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Serikali yaagiza tiba, vipimo malaria bure

UKURASA 2



Wafanyabiashara wadogo 'machinga' wakiendelea na biashara zao kwenye eneo lisiloruhusiwa nje ya kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho mkoani Dar es Salaam jana asubuhi licha ya vibanda vyao kubomolewa juzi usiku. Huku wengine wakiendelea kujenga upya meza zao za biashara. **PICHA: ROMANA MALLYA**

## Panya Road watikisa tena Dar, wajeruhi na kupora

UKURASA 2

# Sheria ya kulinda taarifa binafsi yaja

UKURASA 2

MICHEZO NABI AANIKA SABABU YANGA UK.24 KABWELA UK.18

# Serikali yaagiza tiba, vipimo malaria bure

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameagiza matibabu ya malaria kutolewa bure kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali.

Pia amewataka watoa huduma kuacha kutoza fedha kwa wananchi wanaofika kufanya vipimo vya malaria na kifua kikuu.

Waziri Ummy alitoa maelekezo hayo jana mjini hapo wakati akizungumza na wananchi katika Zahanati ya Disunyara Halmashauri ya Kibaha alipokuwa katika ziara ya siku moja akiambatana na Mkurugenzi wa Mfuko wa kimataifa wa kusaidia mapambano dhidi ya virusi vya (HIV), kifua kikuu (TB) na malaria (Global Fund) Peter Sand, aliyefika kujionea huduma.

"Kipimo cha malaria cha haraka ni (MRDT), dawa za malaria Alu na sindano ya malaria kali ni bure na kipimo cha kifua kikuu ni bure kwasababu ya Global Fund wanatusaidia tuweze kutokomeza magonjwa haya matatu," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), malaria ni miongoni mwa magonjwa sita yanayochangia vifo vingi nchini sambamba na magonjwa ya mfumo wa hewa, kisukari na Ukimwi.

Katika hatua nyingine aliwataka wanaoishi na Virusi vya Ukimwi kutoacha kutumia dawa za kufubaza virusi vya ugonjwa huo (ARV) na pia kusitisha ngono zembe kutokana na kasi ya maambukizi iliyoko kwa sasa.

Kwa mujibu wa Ummy kumekuwapo na kusuasua kwa matumizi ya dawa za ARV kwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi jambo ambalo ni la hatari.

"Kati ya watu 100 Tanzania wanaoishi na virusi vya ukimwi 95 wanatumia dawa tumeona kusuasua kwa matumizi ya ARV kwasababu watu hawaoni kwa hiyo wanaacha kutumia dawa," alisema Ummy.

"Wakati tunakaribia kuushinda Ukimwi, tunaanza kurudi nyuma hata kama huumwi unaona vimepungua tusiache kutumia dawa," alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, alisema Global Fund ndiyo wanaosaidia, na kwamba wanasaidiana na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuboresha huduma za afya.

Kunenge alisema kuwa kiongozi Global amefika kujionea shughuli zinazofanywa na Mfuko huo kwa Tanzania amefika kutembelea baadhi ya vituo vya afya vya mkoa huo.

Mkurugenzi wa Global Fund, Peter Sand, alisema Mfuko huo umeridhishwa na huduma zinazotolewa hususani kukabiliana na magonjwa Ukimwi, malaria, kifua kikuu na huduma za mama na mtoto.

Sand aliwahikikishia kuwa Mfuko huo utaendelea kushirikiana na Tanzania kuendeleza mapambano dhidi ya kifua kikuu, Ukimwi, maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na malaria.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Jim Yonazi (kulia), wakifuatilia kwa makini mada mbalimbali katika mkutano na wadau wa teknolojia ya habari na mawasiliano, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yatoa kibali kutunga sheria kulinda taarifa binafsi

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema wizara yake imepata kibali cha kutunga sheria itakayolinda taarifa binafsi.

Nape, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa siku mbili uliolenga kujadili namna ya kuwaunganisha watu wote kutumia teknolojia kuwasiliana na kupashana taarifa mbalimbali.

Alisema, sheria hiyo itasaidia kuongeza wawekezaji nchini kwa kuwa wengi wao wanapenda usiri wa taarifa zao pamoja na kudhibiti tabia za watu ambao wanapenda kuingilia taarifa binafsi za mtu kwenye mitandao.

"Kwenye Bunge la mwezi huu tunakwenda kusoma kwa mara ya kwanza mswada wa sheria hiyo na baada ya hapo itajadiliwa. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wadau wote kutoa maoni ili kusaidia kuongeza maboresho katika sheria hiyo.

"Sheria hiyo ikishapitishwa na wabunge, Mheshimiwa Rais, ataitia saini mara moja ili ianze kutumika kwa sababu tumeisubiri kwa muda mrefu sana," Nape alisisitiza.

Alisema, mkutano huo ni muhimu kwa Tanzania kwa sababu utaiweka nchi katika kile alichokiita ramani ya dunia na kuchangia kurahisisha mawasiliano kwa kiasi kikubwa.

"Utakumbuka serikali imelenga kujenga uchumi wa kidijitali, uchumi huo hautomwacha mtu nyuma. Kwa hiyo, ni wakati muhimu na watakuwapo kwa siku mbili kujadiliana kuangalia hali ilivyo pamoja na vikwazo vilivyopo.

"Tanzania tunafanya biashara na nchi mbalimbali katika Bara la Afrika, ni wakati muhimu kwetu kupata taarifa kutoka kwa nchi za wenzetu, hivyo hatuna budi kubadilishana uzoefu na wenzetu kupitia teknolojia hiyo," alisema.

Mkurugenzi Masuala ya Kisekta Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Emanuel Manase, alisema mamlaka hiyo na serikali wataendelea kutengeneza huduma wezeshi zitakazomfikia kila mtanzania kuhakikisha kila mtu anapata manufaa ya huduma hiyo.

"Kuwapo kwa huduma za mawasiliano kunafungua fursa za ubunifu na ajira. Katika mnyororo wote huo kuna ajira nyingi zinapatikana kwa hiyo, kupitia mkutano huu tutaendelea kujifunza mengi juu ya njia bora na salama jinsi ambavyo ubunifu unaweza kutuvusha kama taifa na kusonga mbele," alisema.

Mkurugenzi wa Masula ya Ushirikiano wa Vodacom Tanzania, Rosalynn Mworia, alimpongeza Waziri Nape kwa kuweka jitihada za dhati kufanikisha upatikanaji wa sheria hiyo, akibainisha kuwa kukamilika kwa sheria hiyo kutasaidia kuipeleka Tanzania katika ulimwengu wa kidijitali.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau kutoka katika nchi mbalimbali za Afrika zikiwamo Burundi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), na Afrika Kusini.

# Panya Road watikisa tena Dar es Salaam

**Na Romana Mallya**

KUNDI la vijana wahalifu mkoani Dar es Salaam, maarufu panya road, limeutikisa tena mkoa huo wa kibiashara baada ya usiku wa kuamkia jana kuyavamia maeneo ya Tabata Kinyerezi, likijeruhi na kupora mali.

Baadhi ya majeruhi, wakisimulia namna walivyovamiwa, walisema wameibiwa fedha, simu na vitu mbalimbali, huku kukiripotiwa kundi hilo lilivamia nyumba 15 na kujeruhi watu wanne maeneo mbalimbali ya mwili.

Mkazi wa Kinyerezi Kibaga, Temu Njelekela, alisema kuwa baada ya kuwasikia wakati akielekea jikoni kutafuta silaha ya kujihami wakawa tayari wameshaingia wanne ndani na kuanza kumjeruhi sehemu mbalimbali za mwili.

Husna Omary, mkazi mwingine wa mtaa huo, alisema walimchukua mtoto wake, wamkashika eneo la kichwa hadi chumbani na kumlaza kisha wakamwekea panga shingoni na wakataka wapewe pikipiki.

"Mmoja wao alisikika akisema, 'unaongeaje naye taratibu kata panga tunaomba fedha', nikachukua suruali aliyokuwa amevaa mume wangu nikawapa," anasimulia Husna.

Zahour Mohammed alisema walimweleza mke wake kuwa wanafanya hivyo kwa sababu kuna mwenzao ameuawa, hivyo wanalipiza kisasi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kinyerezi, Hashim Fadhili, alisema kundi la vijana zaidi ya 30 walivamia mtaa huo wakiwa na pikipiki sita, mapanga na chupa zilizopasuliwa.

Alisema kutokana na wingi wao, waliokuwapo eneo hilo walijaribu kupambana nao lakini nguvu yao ilikuwa kubwa, hivyo waliwajeruhi baadhi ya wananchi.

Kaimu Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, William Mkonda, akizungumza na Nipashe jana kuhusu tukio hilo, alisema hao ni wahalifu na kuwa jeshi hilo linaendelea na msako maeneo mbalimbali ya Tabata na mkoani Dar es Salaam kwa ujumla.

"Tunawashikilia watu kadhaa, msako mkali unaendelea na tunahamasisha wananchi waweke vikundi vya ulinzi shirikishi katika mitaa yao. Tunafanya doria maeneo yote ya jiji kuhakikisha hali ya utulivu inaendelea, Tabata yote tunaendelea na msako, waliojeruhiwa ni watu wanne," alisema.

Wiki iliyopita, kundi hilo liliripotiwa kuvamia maeneo ya Tabata, likijeruhi na kupora mali.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Waziri wa Kilimo, Uvuvi, Maendeleo ya Vijijini na Misitu wa Serikali ya Ufalme wa Morocco, Prof. Mohammed Sadiki, baada mazungumzo yao, Ofisini kwake, jijini Rabat, nchini Morocco jana. Walijadili kuhusu kuongeza ushirikiano kwenye sekta mbalimbali ikiwemo kilimo na usalama wa chakula. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Saratani ya kinywa janga lingine nchini

**Na Romana Mallya**

MRATIBU wa Afya ya Kinywa na Meno Taifa kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, amesema kwa mwaka jana, takriban wagonjwa 600 waligundulika kuwa na saratani za kinywa na meno.

Dk. Nzobo alibainisha hali hiyo jana mkoani Dar es Salaam katika mahojiano na Nipashe wakati wa Kongamano la Vijana la siku tatu lililoanza juzi, likilenga masuala ya uongozi katika afya ya kinywa na meno na kuwakutanisha washiriki 26 kutoka nchi za Malawi, Rwanda, Tanzania na Zambia.

Kongamano hilo limeandaliwa na mashirika yasiyo ya kiserikali, MC-Tanzania lenye maono kwa jamii ya Tanzania kuishi bila magonjwa ya kinywa na meno na MCW Global la Marekani linalotaka kufikia viwango vya juu vya elimu, afya bora na usalama wa kiuchumi ulimwenguni.

Dk. Nzobo alitaja vyanzo vikubwa vinavyosababisha saratani ya kinywa na meno ni matumizi ya bidhaa za tumbaku ikiwamo uvutaji wa sigara na unywaji wa pombe uliopitiliza.

"Matibabu ya saratani ni kama kawaida, atafika hospitalini atachukuliwa kipimo, hii itajulikana ni saratani ya aina fulani. Matibabu kuna mionzi, kuna kufanyiwa upasuaji au atapewa dawa za dripu au kumeza, atapona lakini endapo mtu atachelewa athari yake ni rahisi kusambaa kwenye mapafu," alisema.

Kuhusu kongamano hilo, alisema wamekutana washiriki kutoka nchi mbalimbali kuangalia shida zinazokabili sekta ya kinywa na meno ili kuzitatua.

"Wataalamu wa kinywa na meno ni wachache, tunahitaji madaktari bingwa angalau 171 lakini mpaka sasa waliopo ni 70 na kati yao, madaktari bingwa 68 wapo hospitali za Dar es Salaam na mmoja Mkoa wa Morogoro na mwingine Dodoma," alifafanua.

Alisema ili kupata madaktari bingwa, uzalishaji wake kwa ngazi ya shahada unatakiwa uwe mkubwa na kwa bahati mbaya awali kulikuwa na chuo kimoja kinachowazalisha na mwaka huu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Kitivo cha Mbeya kimeanza kuchukua wanafunzi ngazi hiyo.

"Tunaomba wazazi na walezi wawatie moyo vijana wao kwamba nchi inahitaji madaktari wa kinywa na meno wengi na eneo hili bado halijatumika vizuri, ni eneo ambalo mwanafunzi akiomba, anapata mkopo," alisisitiza.

Pia alisema kada ya matabibu meno ambao wanaohitajika ni 2,500 na kupitia kibali kilichotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan mwaka huu, zaidi ya matabibu meno 150 wameajiriwa kwenye vituo vya serikali na kufanya jumla yao kwa sasa kufikia 404.

Alisema baada ya ajira hizo kutolewa, hakuna wengine ambao wamebaki na sasa vituo binafsi vina uhitaji wa watalaamu hao.

Pia alisema kati ya vituo 9,726 vinavyotoa huduma ya afya, 597 ndivyo vinavyotoa huduma ya tiba ya kinywa na meno, sawa na asilimia 6.7.

Dk. Nzobo alitaja kikwazo kingine ni uhaba wa dawa na vifaa tiba vya meno hasa kutoka Bohari ya Dawa (MSD).

"Kwa sasa msimamo wa wizara, hatutaki kuwa na taifa la vibogoyo, tunataka Watanzania wabaki na meno yao. Mtu atatibiwa jino linabaki, hii inaboresha afya ya mwili, uking'oa meno kuna baadhi ya vyakula hutaweza kula, wale waliong'olewa meno mengi, ipo huduma ya meno bandia, ambao bado tunakataa vibogoyo," alisema.

Dk. Nzobo alisema huduma hiyo ilikuwapo muda mrefu na watalaamu wa afya ya kinywa na meno wanaifahamu, hivyo katika kuwabana wasiendelee, upo mfumo wa taarifa ambapo mtu akiziba meno ya watu wengi, utatoa alama ya kijani yenye maana nzuri.

"Ukiziba wengi kidogo utakupa alama njano kama utaziba wachache utakuwa umeng'oa wengi mfumo utakupa alama nyekundu, maana yake wewe ni hatari hufai.

"Mfumo huu umeanza kufanya kazi Januari mwaka huu na tayari baadhi ya maeneo watalaamu wameanza kubadilika na matokeo ni mazuri hasa hospitali binafsi. Mfumo unawapima wataalamu wa hospitali za serikali na binafsi," alisema.

Rais wa Chama cha Afya ya Kinywa na Meno Tanzania, Dk. Deogratius Kilasara, alisema mkutano huo ni wa kwanza na wa aina yake kufanyika Tanzania na Afrika uliolenga afya ya kinywa na meno.

"Tumekutanisha vijana kutoka Tanzania, Rwanda Zambia, Malawi, Zimbabwe, Cosovo na Marekani. Mambo ya kinywa na meno siyo kwa Tanzania tu, kwa nchi nyingi ni kitu ambacho hakipewi msukumo wa mambo ya sera za nchi mbalimbali," alisema.

Meneja wa MC-Tanzania, Venance Ngungo, alisema lengo la kongamano hilo MCW Global ni kuboresho masuala ya uongozi katika afya ya kinywa na meno kwa wataalamu wa afya ya kinywa na meno kwa vijana wa Afrika Mashariki na Kusini.

# Bunge laingilia tozo maegesho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeagiza Halmashauri za Manispaa ya Temeke na Kinondoni kuweka utaratibu mzuri wa tozo za maegesho ya magari ili kuondoa malalamiko kwa wananchi.

Jana Nipashe ilichapisha habari kuhusu malalamiko ya tozo hizo kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo wananchi walilalamika kulipishwa tozo katika maeneo ambayo hawajawahi kuegesha kwa kipindi husika, jambo linalowapa usumbufu.

Akizungumza jijini hapa jana baada ya kamati hiyo kukutana na Halmashauri za Manispaa ya Temeke na Kinondoni kuhusu hoja za ukaguzi za mwaka 2020/21, Mwenyekiti wa LAAC, Grace Tendega, alisema kamati imeshauri wakarejee na kuangalia vizuri suala hilo.

"Tunahitaji kweli fedha za kuendesha halmashauri zetu lakini ziwe rafiki kwa wananchi. Kwa hiyo, kuwe na utaratibu mzuri wa kuhakikisha wananchi wanaridhika na huduma inayotolewa na wanaotozwa, ndicho tunachotaka wakitekeleze," aliagiza.

Mwenyekiti huyo alisema wamezitaka halmashauri hizo kuhakikisha zinaweka utaratibu mzuri ambao wananchi hawatalalamikia suala hilo. "Wananchi wanufaike na huduma siyo kuumizwa na huduma," alisema.

**HOJA ZA CAG**

Kuhusu hoja za ukaguzi, Tendega alisema wamebaini Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ina tatizo la makisio ambapo kwa miaka mitatu mfululizo wanafanya makisio ya chini.

"Yaani makisio yao yalikuwa Sh. bilioni 33 kwa mwaka 2020/21 lakini wamekusanya Sh. bilioni 35 na hata miaka ya nyuma walikuwa wanakisia Sh. bilioni 31, wakakusanya Sh. bilioni 36. Kwa hiyo, tumewataka wawe na makisio halali kulingana na fedha wanazokusanya," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kamati hiyo imeagiza kuwekwa makisio makubwa kwenye mwaka wa fedha unaokuja. Pia alisema kamati imeagiza hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa manispaa hizo ambazo hazijafungwa, zifungwe hata kama ni za kisera.

"Tunataka hoja zao sita ifikapo Juni 30, 2023 ziwe zimefungwa," aliagiza. Kuhusu mgawanyo wa asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Manispaa ya Temeke, Mwenyekiti Tendega alisema zaidi ya Sh. milioni 590 hazijarejeshwa.

"Tumewataka wafanye mkakati maalum wa kuhakikisha fedha hizi zinarejeshwa ili kukopesha wanawake wengine, vijana na watu wenye ulemavu," alisema.

Kwa upande wa Kinondoni, mwenyekiti huyo alisema suala la kutoa kwa makundi maalum asilimia 10 ya mapato ni kwa mujibu wa sheria, hivyo wahakikishe wanatekeleza.

Ilibainika Sh. bilioni 1.04 hazijarejeshwa na kuagizwa wazifuatilie zirejeshwe.Tendega alisema Kinondoni pia wanakusanya fedha lakini hawapeleki benki ambapo Sh. milioni 334 zilikusanywa na kuagizwa kuhakikisha zinapelekwa benki haraka na wafuate utaratibu.

Mwenyekiti huyo alisema kamati imebaini timu ya mpira ya KMC inayomilikiwa na manispaa hiyo ilipeleka stakabadhi feki na kuagiza kuwapo na chombo cha usimamizi wa timu hiyo. "Wakiunda hicho chombo kitawasaidia, kujua fedha zipi zimetumika na mapato yanayopatikana," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 09/09/2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 09-09-2022** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DODOMA kuelekea DAR ES SALAAM,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 175 DFN / T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 18.00**
   **Upana** - **mita 2.80**
   **Kimo** - **mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **DODOMA hadi DAR ES SALAAM kupitia MOROGORO.** Gari itasafiri muda wa mchana tu *(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117034802



Wananchi wakiangalia mabaki ya gari aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili T 880 DWD, lililokuwa limebeba magazeti kutoka mkoani Dar es Salaam kuelekea mikoa ya kaskazini baada ya kupata ajali, eneo la Kwedizinga, Wilaya ya Handeni mkoani Tanga jana alfajiri na kusababisha watu wawili kufariki na watatu kujeruhiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawili wafariki dunia ajali ya gari lililobeba magazeti

**Na Oscar Assenga,** HANDENI

WATU wawili wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa baada ya basi dogo aina ya Toyota Hiace, lililokuwa limebeba magazeti kutoka jijini Dar es Salaam kuelekea mikoa ya Kanda ya Kaskazini kupata ajali.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi (ACP), Safia Jongo, jana alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kueleza kwamba ilitokea eneo la Kwedizinga, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga.

"Yes (ndiyo) imetokea ajali hiyo ilikuwa majira ya saa 12:20 asubuhi, wakati hilo basi dogo aina ya Toyota Hiace, lenye namba za usajili T 888 BWD lililokuwa limebeba magazeti, lilikuwa likijaribu kuyapita magari mengine kwa mwendo kasi.

"Kwa bahati mbaya likashindwa kumaliza na hivyo kuligonga kwa nyumba lori la mizigo aina ya Scania, lenye namba za usajili T 287 AVW ambalo lilikuwa limeegeshwa pembeni."

Kamanda Jongo, alimtaja mmoja wa waliofariki ni dereva wa Hiace, Francis Masawe (36).

Kamanda Jongo alisema: "Huyo dereva licha ya kuonywa mara kwa mara na askari wa barabarani, eneo hilo ni hatari kutokana na kuwa na kona kali, lakini alipuuza.

"Ukiangalia ajali hii, chanzo kikubwa ni dereva wa Hiace ambaye alitaka kulipita gari lililopo mbele yake, ndipo alipokutana na lori na kuligonga."

Kwa mujibu wa Kamanda Jongo licha ya eneo hilo kuwa na sehemu ya operesheni za barabarani, kuangalia hali ya usalama, lakini madereva wamekuwa wakitumia muda wa mwisho wa ukaguzi kuvunja sheria za usalama barabarani.

# CRDB yazindua ATM ya kuweka fedha

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Benki ya CRDB sasa wana uhakika wa kupata huduma ya kuweka fedha saa 24 kupitia ATM za kisasa za kuweka pesa baada ya benki hiyo kuzindua.

Ofisa Mkuu Uendeshaji wa Benki hiyo, Bruce Mwile, alibainisha hayo juzi wakati akizindua huduma hiyo katika tawi la Benki ya CRDB Mlimani City.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwile alisema mashine hiyo inatumia teknolojia ya kisasa ambayo inawawezesha wateja kuweka fedha wenyewe bila usaidizi kwa urahisi, usalama na unafuu.

Mwile alisema mashine hizo zina uwezo wa kupokea hadi Sh. milioni 100 kwa mara moja.

"Tunatambua zipo biashara ambazo zinaendeshwa nje ya muda wa kazi wa kawaida ambapo matawi ya benki na hata CRDB Wakala wanakuwa wamefunga, mashine hii inakwenda kutatua shida hii Kwanzaa huduma ya kuweka fedha sasa itapatikana saa 24 kwa urahisi na usalama zaidi," alisisitiza.

Aliongeza: "Pamoja na msisitizo wa mifumo ya kidijitali, ukweli ni kuwa matumizi ya fedha taslimu (noti na sarafu) bado ni makubwa. Hii inaifanya huduma ya kuweka pesa 'deposit' kuwa moja ya huduma muhimu za kibenki.

"Mashine hii ya kisasa ya kuweka fedha iliyozinduliwa na Benki ya CRDB inatarajiwa kuleta mapinduzi makubwa ya utoaji wa huduma."

Akifafanua namna ya kutumia mashine hiyo, Mwile alisema: "Mteja atatakiwa kuchagua lugha anayopenda kati ya Kiswahili na Kiingereza, kisha ataweka TemboCard yake na kuingiza namba ya siri. Mteja ataweka fedha hadi noti 200 na kisha kubonyeza kitufe cha 'Weka Pesa', kisha atapokea taarifa kupitia ujumbe mfupi."

Mwile aliongezea kuwa pamoja na kuzindua mashine hiyo katika tawi la Mlimani City, Benki ya CRDB pia inatarajia hadi ifikapo mwishoni mwa mwezi Oktoba, itazindua mashine nyingine za kisasa zaidi katika miji na sehemu zote zenye biashara kubwa nchini kote ikiwamo Mwanza, Arusha na Dodoma.

Benki ya CRDB inatajwa kuwa benki kiongozi nchini ikiongoza katika ubunifu wa huduma na bidhaa zinazokidhi mahitaji halisi ya wateja.

Benki hiyo inaongoza kwa kuwa na mtandao mpana zaidi wa utoaji huduma kupitia matawi zaidi ya 260, CRDB Wakala zaidi ya 22,000, ATM zaidi ya 550 na vifaa vya ununuzi (PoS) zaidi ya 2,500.

Benki ya CRDB pia inaongoza kwa ubunifu wa mifumo ya kidijitali ya utoaji huduma ikiwamo SimBanking, SimAccount, Internet Banking, na TemboCard.

Mtandao wa benki hiyo pia umevuka mipaka hadi Burundi ambako ina kampuni tanzu na hivi karibuni inatarajia kuingia katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

## Mwanajeshi ajinyonga, aacha ujumbe kwa mke

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKARI wa Jeshi la Anga, Sajenti William Giriango (40), amekutwa amepoteza maisha, akidaiwa kujinyonga kwa kutumia mkanda wake wa suruali kwenye dirisha la nyumba ya kulala wageni iliyoko Mtaa wa Hazina jijini Dodoma huku akiacha ujumbe.

Kamanda wa Polisi mkoani hapo, Martin Otieno, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo juzi mchana kwenye nyumba ya kulala wageni iliyofahamika kwa jina la Morning Star.

"Amejinyonga kwa kutumia mkanda wake wa suruali na kuutundika kwenye dirisha hadi umauti kumkuta," alisema.

Alibainisha kuwa baada ya kupekuliwa, mwili wake ulikutwa na ujumbe.

"Kuna ujumbe wa kwanza alimwandikia mama mzazi ulisomeka 'Mama yangu nisamehe sana ninakuomba', na ujumbe wa pili kwa mke wake unasema 'mke wangu kwako mama Derick nisamehe sana kwa maamuzi haya, maisha kwangu hayana maana tena, nisamehe sana nimejitahidi nimeshindwa ninaomba uwatunze watoto wetu," alinukuu.

Alishauri mtu anapokuwa na msongo wa mawazo, atafute watu wa kuzungumza nao na kubadilishana mawazo.

"Kuliko kufikia uamuzi huu kwa kukaa na kitu kifuani, huwezi kukitoa na kufikia uamuzi wa kujinyonga," alisema.

# Anayedaiwa kujiwasilisha Samia aikana simu kortini

**Na Grace Gurisha**

MJASIRIAMALI Nickson Mfoi (20) anayetuhumiwa kutumia jina la Rais Samia Suluhu Hassan kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, ameishangaza mahakama baada ya kukataa vielelezo vyake ikiwamo simu na laini yake ilhali awali alikubali kukutwa na vitu hivyo alipokamatwa na askari polisi.

Mfoi amedai hayo baada ya kurudishwa mahabusu na kukaa siku saba ambapo Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ilipanga jana kupokea vielelezo vya kesi hiyo baada ya mshtakiwa kuvikubali Septemba Mosi, 2022.

Mshtakiwa huyo alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate, baada ya hakimu kuagiza mshtakiwa kupewa vielelezo vilivyotolewa na Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, ili avione kama ni vyenyewe au la.

Vielelezo alivyopewa mshtakiwa ili avitambue ni simu aina ya Infinix ambayo ndani yake kulikuwa na laini, hati ya ukamataji mali, taarifa ya uchunguzi wa simu anayodaiwa alikutwa nayo, fomu ya usajili wa mtandao wa mteja na maelezo ya onyo.

Mshtakiwa aliposhika simu hiyo, aliigeuza mara mbili kisha akaketi kwenye kiti kizimbani na hapo ndipo Hakimu Kabate akamwambia asimame ili aseme kama ndiyo simu aliyokutwa nayo.

"Siyo yenyewe, mimi nilikubali siku ile kwamba ni kweli nilikamatwa katika Hoteli ya Malaika, ndicho nilichokubali," alidai Mfoi.

Baada ya mshtakiwa kukataa, Hakimu Kabate alisema licha ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali (PH) na kukiri na jana kukataa vielelezo hivyo, anaamuru kesi iendelee kusikilizwa na mashahidi wapewe hati za wito.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Oktoba 18 na 19, 2022 kwa ajili ya kusikilizwa na itatajwa tena Septemba 20, 2022.

Awali, wakati akisomewa PH, mshtakiwa alikubali kwamba alitumia akaunti ya Facebook yenye jina la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na kujipatia Sh. 40,000 kwa njia ya udanganyifu.

Mshtakiwa huyo pia alikiri kwamba Septemba 2021, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nia ya kulaghai umma, alijiwasilisha kama Rais Samia Suluhu Hassan kupitia akaunti yake ya Facebook.

Pia alikiri kwamba Oktoba 2, 2021 alikutwa akitumia laini ya simu ambayo awali ilikuwa inamilikiwa na Getness Jackson kwa madai kwamba alipewa na mtu anayesajili laini.

"Ni kweli hii akaunti ya Facebook nilikuwa ninaitumia mimi, niliuziwa lakini yaliyokuwa yakiendelea humo mimi siyajui na ni kweli nilikuwa ninatumia simu ambayo haijasajiliwa kwa kidole changu," alidai Mfoi.

# Mjema awaonya walimu unywaji pombe kupitiliza

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga amewataka walimu kujiheshimu ili kurudisha hadhi ya walimu iliyokuwapo miaka ya nyuma nchini, akinyoshea kidole tabia za kukesha kwenye baa na kilabu cha pombe za kienyeji kila siku.

Sophia Mjema, alitoa onyo hilo juzi alipozindua vitabu vya mikakati ya kuboresha elimu nchini mkoani humo.

Alisema, hadhi ya walimu ambayo ilikuwapo miaka ya nyuma inapaswa kurejeshwa, akiwa na ufafanuzi kwamba zamani mwalimu alikuwa akionekana mtaani anapewa heshima kubwa, lakini sasa mambo hayapo hivyo tena.

"Zamani ninakumbuka akipita mwalimu mtaani, anaheshimika kweli, utasikia yule mwalimu fulani hata akizungumza jambo kwenye mkutano linazingatiwa, lakini siku hizi heshima hiyo haipo tena, walimu wanalewa tu kwenye baa, wengine wanavaa nguo zisizo na staha yaani vurugu tupu," alionya.

Mjema, pia alikemea suala la viongozi na wazazi kudhalilisha walimu mbele ya wanafunzi na kuagiza kuwa mwalimu akifanya kosa, aitwe pembeni na kuonywa na siyo kudhalilishwa na kushusha heshima yake kwa watoto.

Alisema, mwalimu akidhalilishwa mbele ya wanafunzi, kundi hilo halitampa heshima tena, hivyo kutaathiri mpaka masomo ya darasani.

Akizungumzia vitabu hivyo vya mikakati ya kuboresha elimu nchini, Mjema alisema vimekuja wakati muafaka na vitasaidia kubaini vikwazo vya ukuaji wa elimu na kupanga mipango ya kuitatua ili kunyanyua taaluma ya wanafunzi.

Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako, alisema vitabu hivyo vitaleta chachu ya kukuza elimu na wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao kwa kuwa vinaibua mbinu mbalimbali za kufundisha na kuboresha miundombinu shuleni.



Wakazi wa Mabwepande, Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wakitoka kutafuta kuni jana kwa ajili ya matumizi ya nishati ya kupikia nyumbani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wenye tatizo misuli, viungo kutibiwa bure Muhimbili

**Na Waandishi Wetu**

KUELEKEA kilele cha Siku ya Maadhimisho ya Fiziotherapia Duniani, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) imeanza kutoa matibabu bure kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi ya viungo na misuli.

Kadhalika, itatoa matibabu kwa wagonjwa wenye matatizo ya kifua kulikosababishwa na mlipuko wa UVIKO-19, pamoja na kuwatibia watoto wenye matatizo ya makuzi.

Akizungumza na Nipashe, Mtaalamu wa Matibabu ya Fiziotherapia, Deus Nshanshuku, alisema huduma hizo zimeanza kutolewa jana na zitamalizika kesho.

"Huduma hiyo ilianza kutolewa Septemba 7, ikiwa ni ufunguzi wa maadhimisho hayo ambayo yatachukua siku tatu hadi Septemba 9, mwaka huu, ikiongozwa na kaulimbiu 'Nafasi ya wafiziotherapia katika kuzuia na kutibu maumivu ya viungo," alisema.

Alisema matibabu ya fiziotherapia hayatolewi kwa kupewa dawa bali hutumia njia kama mikono, kufanya mazoezi tiba na kutumia vifaa vya umeme maalum kwa matibabu.

"Matibabu yake hayajawa moja kwa moja kutumia dawa bali mtu huenda kwa mtaalamu wa fiziotherapia ambaye anakuwa na mbinu mbalimbali za kutibu huo ugonjwa ikiwamo mikono yake, vifaa vya umeme maalum kwa matibabu na mazoezi tiba," alisema Nshanshuku.

Vile vile, huduma zilizopewa kipaumbele ni utoaji wa elimu ya tiba ya fiziotherapia kupitia tamasha hilo na vyombo vya habari pamoja na uchunguzi wa magonjwa mbalimbali, kupewa ushauri na wataalamu wa idara hiyo juu ya matibabu ya maradhi ya viungo na misuli.

Mbobezi kutoka Idara Fiziotherapia MNH, Akwilina Antony alisema idara yao inahusika pia na matibabu ya maradhi ya viungo kwa watoto, matatizo katika makuzi yao na kifafa cha mimba kwa wanawake waliotoka kujifungua.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wagonjwa waliofika kupata huduma hizo walishukuru MNH kwa kutoa tiba za magonjwa yasiyo ambukizi bila malipo, huku wakiwashauri wale wenye maradhi ya viungo na misuli kuja kupata huduma hiyo.

Raheem Ally, Mkazi wa Yombo, mkoani Dar es Salaam alisema amefurahi kupata huduma hiyo kwa kuwa amehangaika kupata matibabu ya maradhi ya pingiri na uti wa mgongo bila mafanikio, anaamini kufika kwake hospitalini hapo atapata ufumbuzi wa matatizo hayo.

"Nilivyofika nimepokewa na kupimwa vipimo mbalimbali, nikakutana na mtaalamu na kusikiliza shida yangu katika uti wa mgongo kisha akanipa ushauri juu ya maradhi yangu."

**●Imeandikwa na Said Muhibu, Isiyaka Nyamihasi na Golden Kisapile (TUDARCo)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Waziri Ummy matibabu bure litekelezwe

**JANA** Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alikuwa mjini Kibaha, mkoani Pwani na kuagiza vituo vya afya vya serikali kutoa huduma bure kwa watu wanaokwenda kutibiwa ugonjwa wa malaria.

Pia aliagiza wanaokwenda kufanya vipimo vya ugonjwa huo na kifua kikuu wasitozwe fedha.

Hatua hiyo ya Waziri Ummy imetokama na ziara yake ya siku moja aliyoambatana na Mkurugenzi wa Mfuko wa Kimataifa (Global Fund) wa kusaidia mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (HIV), kifua kikuu (TB) na Malaria, Peter Sand, aliyefika kujionea huduma zinazotolewa na vituo hivyo.

Mfuko huo unasaidia Tanzania kutokomeza magonjwa ya malaria, kifua kikuu na Ukimwi.

Ugonjwa wa malaria ni miongoni mwa magonjwa matano nchini unaoongoza kwa kusababisha vifo.

Hivyo, hatua ya Waziri Ummy kuagiza vituo vya afya vya serikali kutoa huduma bure kwa wagonjwa wa malaria, itasaidia kupunguza vifo.

Ni kweli baadhi ya watu wanashindwa kwenda vituo vya afya kwa kutokuwa na fedha za matibabu na vipimo na kuishia kununua dawa za kutuliza maumivu au kwenda kwa waganga wa jadi.

Magonjwa yaliyotajwa na Waziri Ummy ambayo yanapaswa kutolewa huduma bure, ndiyo yanayoongoza kwa kusababisha vifo nchini.

Kwa mfano ugonjwa wa malaria humaliza damu kwa muda mfupi na mtu asipopata matibabu kwa wakati, hupoteza maisha.

Magonjwa kama kifua kikuu na Ukimwi, dawa zake ni kali hivyo mtu anahitaji kula chakula cha kutosha ili asiweze kupata madhara.

Ukiangalia baadhi ya watu wanaougua maradhi hayo, wanakosa uwezo wa matibabu na lishe nzuri. Hivyo hatua hiyo ya kutoa huduma hiyo bure itawasaidia wananchi wengi ili pesa ambayo alikuwa aitumie kwenye matibabu imsaidie kununua lishe bora.

Kwa wanaotumia dawa za kufubaza virusi vya ugonjwa wa Ukimwi (ARV) wanahitajika kula vizuri ili miili yao iweze kujijenga na kuwa na afya njema.

Ummy katika ziara hiyo alitahadharisha wanaosuasua kutumia dawa za ARV kwa wanaoishi na Virusi vya Ukimwi kuwa ni hatari kwao kwa sababu maambukizi yanasambaa kwa kasi.

Anasema katika watu 100 nchini wanaoishi na virusi vya Ukimwi, 95 wanaotumia dawa wanasuasua kwa kujiona wapo vizuri na hivyo kuacha kutumia.

Aliwakumbusha kuwa hata kama wanaona hawaumwi, wasiache kutumia dawa.

Ni matumaini yetu kuwa agizo hili la Waziri Ummy litatekelezwa ili wagonjwa wanapokwenda kupata huduma wasipate usumbufu.


Uzoefu unaonesha kuwa maagizo mengi yanapotolewa utekelezaji wake huchukua muda na wale wanaohitaji huduma kuona kama wananyanyasika na kudharauliwa.

Utaratibu wa kuviongoza vituo hivyo ufanyike kwa wakati ili vifo vitokanavyo na magonjwa hayo vizuilike.

Mkurugenzi wa Global Fund Peter Sand, akizungumzia mfuko huo alisema ameridhishwa na huduma zinazotolewa hususani kukabiliana na magonjwa ya Ukimwi, malaria, kifua kikuu na huduma za mama na mtoto.

Alihikikisha kuwa mfuko huo utaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza mapambano dhidi ya kifua kikuu, HIV, maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na malaria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wakati mwafaka dawa asilia kuchukua nafasi yake nchini

**TIBA** asili ni hali ya kutumia mitishamba isiyokuwa na dawa kemikali na wakati huohuo, ni chakula cha kujenga mwili na viini vyake.

Kwa mujibu wa takwimu mbalimbali zilizopo, inaonyesha zinatoa mchango mkubwa kwa jamii katika upatikanaji wa matibabu salama kwa njia ya tiba asili.

Hadi sasa kuna hesabu inayotajwa ya dawa za asili 85 zilizosajiliwa tangu Septemba mwaka jana na Baraza la Tiba Asili. Pia, hivi karibuni serikali imeanza kutoa huduma jumuishi za tiba asili na tiba za kisasa nchini katika vituo vya Momela wilayani Meru mkoani Arusha na MaibongSukiDar, Dar es Salaam.

Nikimrejea Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kusirye Ukio, katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika, alipomwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu katika kilele cha maadhimisho hayo ambayo yalifanyika mkoani Morogoro, amenena mambo kadhaa ninayoyaona yana mashiko kitaifa.

Dk.Kusirye anasema, kuanzishwa huduma hizo ni mafanikio makubwa kwani tangu uhuru wa nchi, kuna huduma chanya ya kuboreshwa na kuendelezwa tiba asili.

"Miongoni mwa mafanikio mengine ni tiba asili kutambuliwa katika Sera ya Afya,kutungwa kwa sheria ya Tiba Asili/Mbadala,kanuni na miongozo mbalimbali pamoja na kuongeza kwa tafiti za tiba asili zinazofanywa na vyuo vikuu vya serikali," anasema.

Anafafanua, mchango wa tiba asili umedhihirika zaidi wakati wa mapambano ya maradhi UVIKO-19 na kwamba viongozi wa Serikali za Kiafrika wanawajibika kuona umuhimu wa kuboresha tiba hiyo katika mapambano ya adui maradhi.

"Huduma za tiba asili zilitumika wakati wa UVIKO-19 na zilifanya kazi kubwa sana kuwahudumia wahitaji ambapo dawa takribani 21 za asili zilitumika, kutokana na hilo Watanzania wamekuwa na imani kubwa na huduma za tiba asili," ametamka.

Rai yake nchini katika suala la kuendeleza huduma za tiba asili, mojawapo inajikita kuwa sehemu ya vipaumbele kiserikali sasa.

Kwa upande mwingine, anavutia katika maono yake kwa Waganga wa Tiba Asili, kutengeneza dawa zenye ubora na kuhakikiwa na Mamlaka zinazotambulika ikiwa pamoja na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Anaongeza kuhusu usalama wa dawa zao, zile zilizothibitishwa zina usalama kwa kiwango kinachokubalika na ndizo zinapaswa kusajiliwa.

Hapo akapiga hatua ya kuwataka waganga wa asilia kuacha kuchanganya dawa za kisasa kwenye dawa zinazotengenezwa na kuuzwa kwa wahitaji na kuongeza kuwa Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na taasisi za utafiti na vyuo inaendelea kufuatilia dawa zote za tiba asili zilizopo sokoni.

Hapo kuna angalizo muhimu kwamba, dawa yoyote itakayokutwa imechanganywa na dawa za kisasa, hatua kali zitachukuliwa kwa mmiliki wa dawa husika.

Inavutia pale Mkurugenzi wa Uzamili na Utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Profesa Esron Karimuribo, anasema Tanzania ina mazao mazuri yanayofanya vizuri, yamethibitishwa ubora katika tiba na kuhakikiwa yanafanya vizuri.

Anaendeleza hoja zake za kisomi kwamba, kutolewe elimu kwa wataalamu wa tiba asili na kwa kuanza wamekuja na utaalamu wa vifungashio kwa dawa hizo, pamoja na utoaji dozi kamili ili kupata matokeo mazuri.

Hiyo nayo inaingia katika hesabu ya hatua zaidi kama taifa, tunajumuisha juhudi za tiba asili katika nyendo zetu kusaka afya sahihi.

Ni hoja inayojaziwa na kauli ya Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Tiba Asili/Mbadala, Elizabeth Lema, anayesema kutokana na kutatua changamoto za Baraza hilo, hivi sasa wamewakamata 'vishoka' na matapeli wanaopita kuwasajili waganga hao na hatua kali za kisheria zinachukuliwa dhidi yao.

Nikitanguliza pongezi kwa lile la Lema, nahimiza vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, kuacha matangazo yasiyo na vibali kutoka Baraza hilo na kwamba litaendelea kutoa elimu, ili kuwa na wigo mpana wa kutoa tiba za asili nchini.

## Sekta binafsi zatakiwa kutafuta fursa kimataifa

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, amezishauri sekta binafsi kujielekeza katika fursa zilizoko kwenye soko la kimataifa.

Amesema sekta hizo zinapaswa kuwaza soko kubwa la kimataifa badala ya soko la ndani.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya pili ya mpango wa kuendeleza viongozi wa kada ya juu katika taasisi binafsi unaondaliwa na Maofisa Watendaji Wakuu wa Kampuni Binafsi Nchini (CEOrt).

Katika mahafali hayo wahitimu 30 kutoka sekta binafsi walihitimu mafunzo hayo.

"Sekta binafsi mnapaswa kujielekeza katika uwekezaji wa soko la kimataifa. Mnapaswa kwenda huko na kuwekeza na sio kujielekeza katika soko la ndani pekee," alisema Mafuru.

Hata hivyo, aliipongeza CEOrt kwa kuandaa programu hiyo ya kuwaendeleza viongozi wenye maono na uwezo ambao wanaweza kuipeleka nchi kwenye nyanja za kimataifa.

Alisema miaka ya nyumba wawekezaji walipokuwa wanakuja nchini kufanya uwekezaji walikuwa na wataalamu wao, lakini kwa sasa wanawatumia wazawa katika miradi yao wanayoweza.

"Wawekezaji sasa hawaoni haja ya kuja na wataalamu wao kutoka nje na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji na tunataka taasisi nyingi za nchini ziongozwe na wataalamu wazawa," alisema Mafuru.

Mwenyekiti wa CEOrt, Dadiv Tarimo, alisema wanaelewa pengo lililopo la uongozi na haja ya uwekezaji wa ziada katika rasilimali watu hapa nchini.

Alisema sababu hiyo ndiyo iliyowasukuma kuja na wazo la kuanzisha programu hiyo ya mafunzo ikiwa na lengo la kuwaongezea ujuzi wakuu wa taasisi mbalimbali hapa nchini.

Tarimo alisema: "Programu hii inaungwa mkono na serikali, Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Strathmore kuanzisha programu hiyo mwaka 2019."

"Awamu ya tatu watakuwa na wahitimu 18 watakaopata mafunzo hayo ya uongozi kwamba kati yao 14 ni kutoka sekta binafsi huku wanne wakitoka serikalini.

# RC ashtuka madiwani kukusanya mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewataka madiwani katika halmashauri za mkoa huo kuacha tabia ya kukusanya kodi kwenye vizuizi na kutoa misamaha, badala yake wawasimamie watendaji kufanya kazi hiyo.

Alitoa angalizo hilo juzi alipozungumza na madiwani wa Manispaa ya Singida, Halmashauri ya Mkalama na Halmashauri ya Mkalama kwa nyakati tofauti kwenye vikao vya Mabaraza ya Madiwani ikiwa ni sehemu ya kujitambulisha.

Serukamba alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya madiwani kuwa wakusanyaji kodi na watoaji misamaha ya ushuru katika mageti mbalimbali ya kukagua mazao, jambo ambalo siyo sahihi.

Serukamba alisema vitendo hivyo siyo vya kiadilifu na havipaswa kufanywa na viongozi kama madiwani kwa kuwa vitasababisha washindwe kuwasimamia watendaji hata kama watakuwa na makosa katika kazi zao.

"Diwani ukikusanya kodi, watendaji hawataweza kukuuliza na hataweza kumsimamia mwingine ambaye alikusanya kodi pasipo kupeleka benki na mfano ukimwomba mhandisi akupe mifuko miwili ya saruji, yeye atachukua mitano na hutaweza kumuuliza," alisema.

Aliwataka madiwani kufanya kazi kwa uadilifu na kushirikiana hasa katika miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Serukamba, akizungumzia kuhusu kilimo, aliwaelekeza madiwani wahakikishe wanawahimiza wakulima kupanua maeneo ya kilimo kwa kuwa serikali imeendelea kutoa ruzuku za pembejeo za kilimo.

Aliagiza wakulima wafanye maandalizi ya mashamba mapema ili mvua za kwanza zitumike kwa kupandia kwa kuwa uzoefu wa msimu uliopita ulionyesha kwamba waliowahi kupanda walipata mazao mengi kulinganishwa na waliochelewa kupanda.

Serukamba alisema serikali inatumia fedha nyingi kuagiza mafuta ya kupikia kutoka nje wakati Mkoa wa Singida una uwezo mkubwa kuondoa pengo hilo kwa kuongeza eneo la uzalishaji wa alizeti.

Akiwa wilayani Mkalama, Mkuu wa Mkoa aliwataka viongozi wa eneo hilo kuhakikisha kunajengwa soko la vitunguu ili kuondokana na kero ya walanguzi kuwafuata wakulima mashambani.

Alisema kwa kuwaacha walanguzi kuingia mashambani kumesababisha wakulima kutopata faida inayotokana na kazi yao kwa sababu ya ulanguzi unaofanywa huko shambani.




Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara wakiwa katika picha ya pamoja na mameneja na maofisa wa Tembo Nickel, walipofanya ziara ya mafunzo katika eneo la mradi huo wilayani Ngara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msumbiji yaja kupata uzoefu usimamizi mawasiliano TCRA

**Na Frank Monyo**

MENEJIMENTI ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Msumbiji (INCM), imefanya ziara nchini ikiwa na lengo la kujifunza masuala ya usimamizi wa mawasiliano kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Ziara hiyo imehusisha maeneo ambayo Tanzania imepiga hatua, hasa usimamizi wa masafa, ubora wa huduma na mawasiliano katika maeneo ya mipaka.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara hiyo, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa INCM, Mhandisi Francisco Chate, alisema wana matumaini ya kujifunza uzoefu kutoka TCRA kusimamia teknolojia na huduma za mawasiliano katika ukanda wa Afrika. "Lengo letu ni kuhakikisha nchi yetu inaunganishwa vilivyo na mawasiliano na ndiyo sababu ya ujio wetu Tanzania, tukiamini TCRA mnao uzoefu wa kutosha kutupatia maarifa zaidi ya namna tunavyoweza kusimamia na kuboresha huduma za mawasiliano hasa simu na mtandao," alisema Mhandisi Chate. Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, John Daffa, ambaye aliwapitisha wajumbe hao katika vitengo mbalimbali ndani ya TCRA alieleza kuwa wapo tayari kushirikiana na INCM kuwapa uzoefu utakaowasaidia kuboresha huduma za mawasiliano nchini mwao.

"Tuna uhakika ushirikiano huu ni muhimu katika kukuza sekta za mawasiliano kwenye nchi zetu na bila shaka wataalamu wetu watawapatia uzoefu mzuri wa namna sekta pana ya mawasiliano inavyosimamiwa," alisema Daffa.

Kwa upande wa Mkuu wa Idara ya Ufuatiliaji na Ubora wa Huduma INCM, Edmundo Alberto, alieleza kufurahishwa na namna TCRA ilivyojizatiti kusimamia sekta ya mawasiliano kwa teknolojia ya kisasa zaidi.

Ziara ya wajumbe wa INCM ni ya pili kufanywa ikiwa na dhumuni la kufanya mageuzi, huduma za mawasiliano nchini Msumbuji.

# LAAC yanusa harufu ufisadi halmashauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imenusa harufu ya ubadhirifu wa fedha katika miradi minane ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, kutokana na kutopata maelezo ya mchanganuo wa matumizi ya fedha husika.

Kutokana na hali hiyo, imetoa miezi mitatu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Selemani Zedi, alibainisha hayo juzi baada ya kukutana na uongozi wa halmashauri hiyo kupitia hoja za ukaguzi za mwaka 2020/21.

"Miradi hiyo ni fedha za uendeshaji wa elimu ya msingi, sekondari, fedha za ujenzi wa zahanati, ujenzi wa vituo vya afya, mfuko wa pamoja wa afya (Busket Fund), elimu kwa matokeo (EP4R), fedha za mradi wa chakula (ERPP), na fedha kwa ajili ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza (NTD)," alisema.

Alibainisha kuwa halmashauri hiyo imeshindwa kuieleza kamati kwamba walianza mwaka na fedha na kiasi gani, kama walikuwa na bakaa, kwa muda wa mwaka mzima walipokea kiasi gani kwa miradi hiyo, wametumia kiasi gani na kama kuna salio au bakaa.

"Kwenye miradi minane wameshindwa kabisa kutuelezea kwamba walipata kaisi gani, ikatumika kiasi gani na mwisho wa mwaka kimebaki kiasi gani. Sasa hapo maana yake ni kwamba kuna mwanya wanaficha au kuna ubadhirifu na upotevu, maana hakuna mantiki yoyote ya kuficha miradi," alisema.

Kiongozi huyo wa kamati alisema, ukaguzi huo utafanyika kwa mradi mmoja mmoja kwenye miradi minane ambayo halmashauri hiyo imeshindwa kutoa maelezo ya mchanganuo wa miradi hiyo. "Kwa mwaka wa fedha 2020/21, walitekeleza miradi 13 ambapo kati ya hiyo, mitano wametoa mchanganuo unaoridhisha lakini miradi minane imeshindikana kuonyesha mchanganuo wa miradi, ni kwamba wanaelezea miradi hiyo wakati mwaka wa fedha unaanza walikuwa na bakaa iliyokuwa nyuma yake kulikuwa na kiasi gani, mwaka mzima wamepata kiasi gani na matumizi yapoje na kama mwisho wa mwaka kuna salio lilibaki?" alihoji.

Zedi, alisema kamati imetoa muda huo kwa CAG kwenda kukagua na kuwasilisha majibu.

"Ninahisi kuna shida ya uwezo wa Mhasibu wa Halmashauri ya Kilosa, maana miradi mingine michanganuo huandaliwa vizuri lakini hii imekuwa tofauti," alisema.




Ofisa Masoko wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Dorothea Lymo, akimsikiliza mmoja wa wateja wakati wa semina maalum ya wastaafu iliyoandaliwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwapa elimu ya kifedha pamoja na kuwaaminisha kuwa kustaafu sio mwisho wa ndoto zao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

**NOTICE FOR CONVENING OF THE 24TH NATIONAL GENERAL CONVENTION**

The President of the Media Council of Tanzania (MCT), does hereby pursuant to Article 13 of the MCT Constitution give notice to members of MCT that the 24th National General Convention (NGC) of the Media Council of Tanzania (MCT) shall be held in Dodoma, on September 28, 2022 at 10.30 am.

The proposed agenda at the 24th NGC is as follows:

1. Opening;
2. Adoption of Agenda;
3. Confirming Minutes of the 23rd National General Convention held virtually from Julius Nyerere International Convention Centre, Dar es Salaam on September 30, 2021;
4. Matters arising from the 23rd NGC;
5. Report of the Executive Secretary;
6. Adoption of 2021 Audited Financial Statements;
7. Appointment of External Auditor for the period ending December 31, 2022;
8. A.O.B;
9. Closing.

MCT members who have not paid their annual subscription fees during the prescribed time are hereby reminded to do so promptly.

**Judge Juxon I. Mlay**
**President**
**Media Council of Tanzania (MCT)**

617036002

# Bunge lataka kasi SGR

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), imelitaka Shirika la Reli Tanzania (TRC), kutumia ujuzi walioupata kwenye utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Reli ya Kisasa (SGR) ili kuongeza kasi kwenye awamu zingine.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, aliagiza hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kupokea na kuchambua taarifa ya utendaji kazi wa shirika hilo.

"Kamati inataka TRC kuhakikisha pamoja na kuwapo na makandarasi wa kigeni kwenye utekelezaji mradi huu, pia inatakiwa makandarasi wazawa wanufaike nayo na fedha zao zilipwe kwa wakati," aliagiza.

Pamoja na hayo, Silaa, alisema PIC imeagiza tija ya uwekezaji kwenye utekelezaji wa miradi hiyo ionekane kwa kuwa kamati hiyo ipo tayari kushirikiana na TRC kushauri zaidi.

"Awamu ya kwanza Dar es Salaam-Morogoro kilomita 390 imebaki asilimia nne, Morogoro-Matukupora kilomita 422 inaenda vizuri kwa asilimia 95, Makutupora-Tabora kilomita 368 mkandarasi yupo 'site' (eneo la mradi), mkataba ulishatiwa saini wa Tabora-Isaka kilomita 165 na mkandarasi wa Isaka-Mwanza wa kilomita 41 yupo site. Kwa hiyo awamu ya kwanza inaenda vizuri," alisema.

Silaa, alisema agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, la kutaka reli ifike mwisho kipande cha Tabora-Kigoma cha kilomita 506 ambacho kipo kwenye mchakato wa ununuzi, Uvinza-Mongati-Gitega, Burundi na chenyewe kitajengwa kwa wakati ambapo zabuni imeshatangazwa na Agosti 9 mwaka huu na mapitio ya makandarasi waliiomba kazi hiyo yatafanyika.

"Reli hii ikifika Mwanza, Kigoma na Burundi itabeba uchumi wa taifa kwa kuwa mizigo inayoingia bandarini ikipata usafiri wa uhakika wa reli itafika kwa haraka, leo yapo maeneo ya Kongo ambayo kutoa kontena kwa Dar es Salaam hadi huko ni dola za Marekani 5,000 ambalo limekuja kwa dola za Marekani 6,000 kutoka China mpaka hapa nchini, kwenda na kurudi," alisema.

Alisema ujenzi ukikamilika, kutakuwa na unafuu wa kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine na hata kupunguza bei ya mbolea na saruji, hivyo gharama za maisha nazo zitapungua.

"Tumewapa maelekezo TRC ya kwenda kuongeza kasi katika hayo maeneo ili tuone reli yetu inaanza kufanya kazi na kutoa huduma kwa siku za karibuni," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema amepokea maagizo yaliyotolewa na kamati hiyo na watakwenda kuyafanyia kazi kwa lengo la kuhakikisha reli inakamilika kwa wakati na inafungua milango ya kibiashara na nchi jirani.

"Kamati imetutaka tuwe na mipango ya kibiashara ili ujenzi ukikamilika, mizigo ipite katika Bandari ya Dar es Salaam, hivyo tumeanza mazungumzo na mashirika yanayochimba madini mfano nchi za Rwanda, Burundi, Zambia na Congo ili kuwa na uhusiano nao, tukikwenda kule tusionekane kama tunakwenda kuchukua tu, bali wote tufaidike maana pale Kongo kuna ujenzi wa Km 160 za reli utafanyika," alisema.

Kadogosa, alisema tayari wafanyakazi wa TRC na bandari wako Kongo kwa lengo la kufanya kazi na utekelezaji wa agizo la Rais Samia la kufungua nchi.

# Bunge laagiza kasi mchakato kuhamisha umiliki ndege ATCL

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), imeagiza serikali kuharakisha mchakato wa kuhamisha umiliki wa ndege 11 kutoka Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA), kwenda Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ili kuondokana na tatizo la mtaji hasi wa Sh. bilioni 239.

Katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ya mwaka 2020/21, ilibainika kuwa ATCL ina madeni makubwa kushinda mali zake.

Akitoa agizo hilo juzi baada ya kukutana na TGFA na ATCL, Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, alisema ndege hizo 11 zina thamani ya Sh. trilioni 1.47, hivyo mali hizo zikihamishwa zitasaidia kuondokana kuwa na mtaji hasi na kukodisha kwa gharama kubwa.

"Mtaji hasi ni Sh. bilioni 239 yaani shirika lina madeni makubwa kushinda mali zake na ndilo eneo lililotajwa zaidi na CAG akikabidhi ripoti yake.

"Kamati inamshukuru Rais (Samia Suluhu Hassan) kwa kutoa agizo la hizi ndege 11 umiliki wake uhamie ATCL. Ina maana ukihamisha ndege unatatua lile suala la mtaji hasi ambapo mali sasa zinakuwa juu ya madeni na kuwa na mtaji chanya," alisema.

"Hivyo tatizo la mtaji hasi linakuwa limeondoka, la pili unaiondolea ATCL gharama kubwa ya ukodeshaji wa ndege kwenye wakala wa ndege za serikali. Sasa ukileta huo mtaji na kuondoa matumizi ya kukodisha maana yake kwa miaka minne mfululizo ATCL ingekuwa inaingiza faida," aliongeza Silaa.

Alisema, kwa mwaka 2021/22, ATCL ingepata faida ya Sh. bilioni 37 na ingepata faida ya Sh. bilioni 18 kwa mwaka 2021 na mwaka ulioishia 2020 ingepata faida ya Sh. bilioni 10.

"Pia shirika limekuwa likipata ongezeko la mapato kuanzia 2017/18 walipata Sh. bilioni 53, 2018/19 Sh. bilioni 111, 2019/20, Sh. bilioni 157, mwaka 2020/21 ilipata Sh. biilioni 174.5 na 2021/22 imepata Sh. bilioni 239.

"Ukiangalia wanafanya vizuri na hasara imekuwa ikipungua, walianza mwaka 2018/19 hasara ilikuwa Sh. bilioni 48, mwaka 2020/21 Sh. bilioni 36, mwaka 2021/22 ilikuwa Sh. bilioni 27," alisema

Aidha, alisema kila siti ya ndege inavyoingiza faida imeongezeka kutoka Sh. 251,000 kwa mwaka 2019/20 hadi Sh.283,000 kwa mwaka 2020/21.

"Hesabu walizofunga 2020/21 wamefunga na faida ya Sh. bilioni 45 ikilinganishwa na Sh. bilioni 18 za mwaka uliotangulia," alisema.

Pia, alisema alisema kamati imeagiza ATCL, itengeneze ripoti ya kuonyesha shirika linasaidiaje taifa kwenye utalii, kilimo, utendaji wa serikali, na biashara.

## Raia Uganda mbaroni tuhuma za kumiliki mihuri ya serikali

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia raia wa Uganda kwa tuhuma za kumiliki na kutumia mihuri mitatu ya serikali kinyume cha sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapo juzi, Kamanda wa Polisi mkoani humo, William Mwampaghale, alisema mtuhumiwa huyo alikutwa akitumia mihuri hiyo kugonga kwenye nyaraka mbalimbali.

"Huyu mtuhumiwa aligonga hizo nyaraka kuonyesha kuwa zimeidhinishwa na idara husika ya serikali kwa maana nyingine zipo tayari kutumiwa na wafanyabiashara kuvusha mizigo mbalimbali nje ya nchi kupitia mpaka wa Tanzania na Uganda-Mtukula, hii tuligundua baada ya kupata taarifa," alisema Mwampaghale.

Alisema kutokana na taarifa hiyo jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama viliandaa mtego na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa. Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Septemba Mosi, mwaka huu, majira ya 11:30 jioni katika kijiji cha Mutukula, Wilaya ya Missenyi akiwa na mihuri mitatu.

"Mihuri hiyo ni ya ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kilimo na Mionzi na katika mahojiano mtuhumiwa alikiri kutumia nyaraka bandia kuvusha magari mbalimbali kwenda nchini Uganda," alisema Mwampaghale.

Aliongeza kuwa kabla ya kukamatwa mtuhumiwa huyo alifanikiwa kuvusha magari 11 na uchunguzi unaendelea ili kubani mtandao wote wa wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu.




Wasamaria wema wakisaidia kuondoa vyombo na baadhi ya vifaa vya Abdalah Hassan (mwenye kipaza sauti mgongoni), aliyehamia na kuweka makazi yake katikati ya Barabara ya 15, jijini Tanga kwa takribani wiki moja sasa, akidai kufikisha ujumbe kwa Serikali kuhusu ugumu wa maisha. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Wakazi Dar waongezwa huduma usafiri daladala

**Na Beatrice Moses**

WAKAZI wa Dar es Salaam wanaendelea kuongezewa huduma ya usafiri wa daladala kwenye maeneo yao na kuwarahisishia maisha.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, akizungumza na Nipashe juzi alisema wamekusudia kuhakikisha huduma ya usafiri inaimarika kila mahali ili kuwawezesha wananchi kupata nafasi nzuri ya kushiriki kwenye shughuli zao za kujitafutia kipato na nyingine za kijamii.

"Baada ya kupokea maoni kuna njia mpya kadhaa daladala zimeanzishwa na bado tunaendelea kupokea maoni tutayafanyia kazi nia ikiwa ni kuhakikisha huduma inapatikana kila panapostahili," alisema Suluo.

Akifafanua kuhusu maboresho hayo, Ofisa Mfawidhi LATRA, Mkoa wa Dar es Salaam, Rahim Kondo alitaja njia hizo mpya kuwa ni Mbezi-Mnazi Mmoja kupitia kwa Mkuwa, Maji Chumvi, External, Mandela,Uhuru na via Mabibo, Kawawa, Uhuru tayari zimeshapata magari 40, wakati Msingwa-Makumbusho na Msingwa-Kawe, zina magari manne kila safari na kufanya jumla kuwa manane.

"Nyingine ni Kigamboni-Mbagala Rangi Tatu kupitia Kisiwani ambayo imeshapata magari 10, ipo ya Mloganzila-Makumbusho kupitia Makongo Juu, hadi sasa ina daladala mmoja kama Simu 2000-Mloganzila kupitia Makongo Juu gari moja," alisema.

Alitaja njia nyingine mpya ni Mbezi-Simu 2000 via Makongo Juu yenye gari moja, Kigamboni wilayani-Machinga Complex, magari mawili, Vikunai-Stesheni, magari 12.

Alisema kuwa kuna baadhi ya njia wamiliki wa daladala wamekuwa mwitikio mzuri, LATRA inaendelea kuhamasisha pia njia zingine ziweze kupata gari za kutosha, lakini wakizingatia vigezo, gari yenye uwezo wa kubeba kuanzia abiria 26 ndizo zinaruhusiwa kuomba njia hizo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Daladala (DARCOBOA), Sabri Mabrouk, akizungunzia kuhusu njia hizo alisema ni jambo linalowafurahisha wamiliki hao kwa kuwa linatanua wigo wa biashara na kufanya izidi kutanuka ikilinganishwa na ilivyoanza.

"Dar es Salaam ina wakazi wengi majibu ya sensa ndiyo yatatupa idadi kamili, wengi miongoni mwao wanategemea usafiri wa daladala, maeneo ya makazi nayo yameongezeka kwa hiyo tunafurahia kutanua huduma yetu ambayo ni biashara," alisema Mabrouk.

"Kutembea mwendo mrefu ili kupunguza gharama za kuunganisha magari inachosha, lakini kuunganisha magari ili kufika eneo kama la Ilala au Buguruni Sokoni kuchukua bidhaa za kuuza ni gharama ikilinganishwa na kipato kidogo ninachopata kulingana na biashara ya genge ninayofanya," alisema Isiaka Yusuph, mkazi wa Mbezi.

Naye Mkazi wa Kimara Yunis Samson alisema kabla ya kuanzishwa kwa safari hiyo ya Mbezi-Mnazi Mmoja ilikuwa ni kero inapotokea kuwa na mgonjwa katika Hospitali ya Amana kwa kuwa ilikuwa ni lazima kuunganisha usafiri ili kufika.

# Mganga wa kienyeji jela kwa kuua akigombea mwanamke

**Na Pilly Kigome**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu kifungo cha miezi 12 jela mganga wa kienyeji, Ismaili Ramadhani, baada ya kupatikana na hatia ya kuua bila kukusudia wakati akigombania mwanamke.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Minde, baada ya mshtakiwa kukiri kosa la kumuua bila kukusudia Mohamed Kamogera.

Akisoma maelezo katika shtaka hilo Wakili wa Serikali, Mosie Kaima, alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Novemba 13, mwaka 2015 maeneo ya Vingunguti Mjimpya, Ilala jijini Dar es Salaam.

Alidai tukio hilo liliitokea majira ya saa mbili usiku wakati mtuhumiwa na Kamogera wakigombania mwanamke.

Aliendelea kudai mahakamani hapo kuwa Kagomera alikuwa anamtuhumu mshtakiwa kuwa ana mahusiano na mwanamke huyo na kukataa tuhuma hizo. Alidai, katika ugomwi huo Kagomera aliambatana na wenzake wanne na kumvamia mshtakiwa wakiwa na mapanga na kumpiga.

Wakili alidai wakati ugomvi huo unaendelea alitokea mtu mmoja aliyetambulika kwa jina la Ali, na kumrushia kisu mshtakiwa ili aweze kujitetea ndipo mshtakiwa huyo alipochukua kisu hicho na kumchoma Kagomera katika mkono wake wa kushoto na kuanguka chini na baadaye kupoteza maisha. Wakili upande wa utetezi, Yohana Maiko aliiomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake kwa kuwa tayari ameshakaa ndani zaidi ya miaka saba na bado kijana mdogo nguvu kazi ya taifa ikiwamo na kutegemewa na wazazi wake.

Alidai wakati wa tukio hilo mteja wake alikuwa na umri wa miaka 20, ni kosa lake la kwanza na hana rekodi yoyote la kosa la jinai.




Mwanzilishi mwenza wa vitabu vya Big Bad Wolf, Andrew Yap (kushoto), ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Big Bad Wolf Sharjah akiwa na mwakilishi wake hapa nchini, Mohamed Noor Hers, wakionyesha kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, sehemu ya vitabu hivyo 500,000 walivyoingiza nchini. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## CUF yawapitisha 12 kuwania ubunge EALA

**Na Loyce Cyriacus, SJMC**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimepitisha majina 12 ya wanachama watakaowania nafasi ya ubunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA).

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano kwa Umma wa CUF, Mhandisi Mohamed Ngulangwa, alisema majina hayo yalipitishwa na Baraza Kuu la CUF lililokaa kikao Agosti 22 na 23, mwaka huu.

Mhandisi Ngulangwa, alisema idadi hiyo itawekwa katika makundi manne na kila kundi litakuwa na wagombea watatu.

"Baraza Kuu la CUF lilipitisha majina ya watu 12 kuwa wagombea katika makundi manne yalioainishwa na kamati ya uongozi, kila kundi kutoa wagombea watatu kwa nafasi moja," alisema.

Ngulangwa, alisema Baraza Kuu la CUF lilipitisha wagombea katika makundi manne ambayo ni ya Zanzibar, Tanzania Bara, Wanawake na wapinzani.

Mhandisi Ngulangwa, aliwataja waliopitishwa ni Habib Mnyaa, Mohamed Ngulawa, Zainabu Mndolwa, Juliet Lugembe, Zainab Ham, Mashaka Ngole, Thomas Malima, Mneke Jaffar, Husna Bakari, Anderson Ndambo na Sonia Magogo.

Katika Bunge la EALA, Tanzania inatakiwa kutoa wabunge tisa kupitia vyama vyenye uwakilishi bungeni.

Hadi sasa vyama vyenye uwakilishi bungeni ikiwamo CCM, ACT-Wazalendo vimeanza mchakato wa kuwapata wawakilishi wao, isipokuwa CHADEMA ambao hawakufanya mchakato huo.

Kwa chama cha ACT-Wazalendo kimewapitisha Ado Shaibu na Pavu Abdallah kuwania nafasi hizo, huku CCM ikiwa katika mchakato wa mchujo wa makada 450 ili kuwapata wawakilishi.

# Timu kuchunguza mikopo elimu ya juu yaanza kazi

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU iliyoundwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kuchunguza utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha wa 2017/18 imeanza kazi rasmi.

Akizungumza juzi katika kikao cha uzinduzi wa timu hiyo, Waziri Mkenda alisema inapaswa kufanya na kukamilisha jukumu hilo ndani ya mwezi mmoja.

Timu hiyo ya watu watano inaongozwa na Prof. Allan Mushi, kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro. Wajumbe wake ni Idd Makame kutoka Zanzibar, na Dk. Martin Chegeni, ambao wote ni wataalamu wa mifumo waliobobea katika sayansi ya kompyuta na takwimu.

Prof. Mkenda, akitangaza kuanza kwa kazi hiyo katika ukumbi wa mikutano wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu HESLB wakati wa kikao kazi cha Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya HESLB, alisema lengo ni kuhakikisha malalamiko yanayotolewa kuhusu Bodi ya Mikopo yanapatiwa ufumbuzi.

Waziri Mkenda, amesema imeongeza bajeti kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu hadi kufikia Sh. bilioni 570, za mikopo kwa wanafunzi, hivyo ni lazima kuwe na usimamizi wa uangalizi wa hali ya juu.

"Hatufanyi hivi kwa sababu ya kuumbuana ila ni kwa sababu ya kutaka uwazi na uwajibikaji na kwa sababu hiyo ni lazima kutoa mikopo kwa haki na vigezo stahiki vilivyowekwa na serikali bila kujuana," amekaririwa Waziri Mkenda.

"Shunguli za elimu zinahitajika kwa kila mtu, hivyo ni wajibu wetu kufanya kwa haki na uwajibikaji uliotukuka. Hatutatoa mikopo kwa kujuana kwa undugu, urafiki au ujamaa hakuna, tunataka haki."

"Na kwenye hili tunakaribisha watu watoe taarifa kwa sababu kama kuna mtoto wa Mkenda uliyesoma naye utakuwa unamjua baba yake ni nani na uwezo wake, halafu wewe unaona mtu huyo amepewa mkopo toa taarifa," alisisitiza.

Prof. Mkenda, alisema mtu yeyote ambaye ana wasiwasi na utoaji wa mikopo anakaribishwa ili kuisaidia timu kufanya kazi yake kwa kuwa na taarifa zenye usahihi wa hali ya juu kutoka kwa wananchi husika.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 8, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



## Maradhi ya akili yalivyofika mbali, kila mmoja sasa wa kujitathmini

Ukurasa 14



## MTIKISIKO TB ILIYOENEA MPANDA
## Umma kuabudu 'manyanga', serikali yaingia ubia na waganga wa jadi

Ukurasa 12

# UTUNZAJI WA NGOZI YA MAFUTA NA JINSI YA KUEPUKA KUPATA CHUNUSI



Hali ya chunusi kwenye ngozi.**PICHA: MTANDAO.**

**Na Dk. Mussa Zaganza**

MARA zote ngozi ya mwili yenye mafuta kwa kawaida huwa inang'ara, nene na yenye rangi iliyotitia. Mara nyingi ngozi yenye mafuta mengi sana, huwa na chunusi nyingi na vipele na mara nyingine huwa na chunusi zenye vichwa vyeusi.

Katika aina hiyo ya ngozi, mafuta hutokana na tezi iitwayo 'sebaceous' na kuzalisha mafuta zaidi ya kiwango kinachotakiwa. Mafuta hayo husambaa katika ngozi na kuifanya iwe na mafuta mafuta.

Sababu zinazofanya ngozi kuwa na mafuta zinajumuisha urithi wa asili; lishe iingiayo mwilini; kiwango cha homoni mbalimbali mwilini; na ujauzito kwa mwanamama.

Mengine ni matumizi ya vidonge vya kuzuia mimba kwa mwanamama; baadhi ya vipodozi anavyotumia mtu; hali ya unyevu (humidity) mwilini, pia hali ya hewa ya joto inapokuwepo mahali hapo.

**FAIDA, HASARA ZA MAFUTA**

Faida kubwa ya kuwa na ngozi yenye mafuta ni kwamba, haizeeki haraka, ikilinganishwa na aina nyinginezo za ngozi.

Upande wa hasara ni kwamba, ngozi ya mafuta inaongoza katika kushambuliwa na magonjwa, ikiwemo chunusi, kwani ni rahisi kuziba vinyweleo vya ngozi

**NAMNA YA KUITUNZA**

Miongoni mwa mambo yanayosaidia kuitunza ngozi yenye mafuta, pia kuepusha chunusi na hali isiyopendeza ni:

Moja, ngozi yenye mafuta inahitajika kusafishwa vyema kwa maji ya moto na sabuni, ili kuzuia vinyweleo visizibwe na mafuta.

Pili, kuepushwe vifaa vigumu visikwaruze uso wako na kufanya hata ngozi ikabanduka, kwani suala hilo husababisha tezi za mafuta kufanya kazi zaidi, ili kujaza sehemu iliyopoteza mafuta.

Tatu, ni jukumu la kuepuka kutumia vipodozi vinavyoifanya ngozi ipoteze maji au kukauka (hasa vipodozi kemikali), kwani vinasababisha sehemu ya juu ya ngozi inyauke na kusababisha mafuta kuziba vinyweleo na kuifanya kutokea vichwa vyeusi.

Nne, mtu anatakiwa ajitahidi kuitunza vyema ngozi yake na kuisafisha vizuri, akiosha uso wake mara moja au mbili kwa siku. Pia, mtu asioshe mara nyingi, kwani kufanya hivyo kunafanya uso kutoa mafuta zaidi ya ziada.

La nne ni kwamba, mtu anapaswa kuchagua kile anachosafishia kwa makini, ajiepushe kutumia 'cream' nzito nzito au vifaa vigumu wakati wa kuosha uso wake.

Inashauriwa kiafya, ni bora kutumia sabuni za kawaida zisizokuwa na dawa. Mtu anaweza kutumia losheni ya kuua bacteria au sabuni zisizo na dawa nyingi (lightly medicated) au sabuni zenye madini mbalimbali. Mtu anapaswa kuepuka kuosha kwa kutumia lotion au michanganyiko yenye alkoholi ndani yake.

Sita, kuna suala muhimu la kutumia maji ya moto au vuguvugu wakati wa kuosha uso; na saba, kuna haja ya kutumia maski za udongo (clay) na tope (mud) kwa kuwa zinasaidia ngozi. Ni bora kutumia maski mara moja au mbili kwa wiki.

***Taasisi ya Natural Skin Solution, ina ufafanuzi wake katika mfumo wa mtandao' online clinic' kwa ajili ya kuwasaidia watanzania kufikia afua ya ngozi na nywele. Wasiliana nasi kwa kupiga au kuchati na whatsapp kwa namba (+255) 0713-039 875 kupata ushauri wa bure na tiba asilia au ufafanuzi wa changamoto katika maeneo hayo.***

AFYA

## MTIKISIKO KIFUA KIKUU ILIYOENEA MPANDA

# UMMA KUABUDU 'MANYANGA', SERIKALI YAINGIA UBIA NA WAGANGA WA JADI

- Ndoa zavunjika kwa kisa 'mkosi TB ya mtoto'
- Mzazi azuru waganga sita kunusuru kichanga
- Asimulia mazito kijinsia, gharama nzito tiba jadi
- Mratibu TB: Tumewaibua 430 na tumenuia zaidi

**Na Neema Hussein, Mpanda**

MTU anaweza kuhoji mazingira ya kuwa na maradhi kifua kikuu? Jibu ni wadudu wanaoambukiza walioko kwenye hewa na mwilini wanakaa kwenye mapafu.

Mganga Mkuu Manispaa ya Mpanda Dk. Paulo Swakala, anafafanua kinga za mwilini kazi yake kubwa ni kuzuia wadudu hao wasisababishe madhara au inawaua.

Anasema mtu anaanza kuumwa pale kinga mwilini zikiwa zimeshuka. Hapo, nako kuna vitu vingi vinavyosababisha kinga kushuka, ikiwemo uzee na aina ya chakula atumiacho, maradhi kama Ukimwi, kansa na kisukari navyo vinachangia, ingawa wakazi wengi wa Mpanda mkoani Katavi, wanaamini zaidi katika ushirikina

Dk. Swakala anawaondoa hofu kwamba kifua kikuu au TB inatibika kwa dawa za hospitalini, kinyume na imani ya dawa za kienyeji. Anafafanua:"Wapo wengine tunawafuata huko huko kwa mganga wa kienyeji unakuta wagonjwa wamelazwa, lakini dalili zote walizo nazo ni za TB.

"Kwa hiyo, mnaongea na mganga wa kienyeji, mnamchukua mgonjwa na kumleta kwenye huduma na wapo wengi ambao wamesaidiwa kwa staili hiyo," anasema.

Nipashe inahoji sababu ya kundi kubwa linaloshuhudiwa kutibiwa kwa waganga wa jadi, Dk. Salawaka akiwa na majibu:"Sio kwamba waganga wana nguvu zaidi kuliko madaktari, hapana! Isipokuwa mgonjwa anatafuta sehemu ambayo anaweza akafika kiurahisi. Kwa hiyo, mganga wa kienyeji ni rahisi zaidi.

"Wapo ambao imani yao inawatuma TB inatibika huko na sisi tunaendelea na juhudi za kufundisha na kuelimisha, kuhakikisha kwamba hawa ambao wanakwenda kwa mganga wa kienyeji, tunawafikia na hatimae kuwatoa.

"Hawa waganga wanafanya ushirikiano na watoa huduma wetu ambao sio waaminifu, wanaiba dawa za TB hizo hizo, wanaenda wanazisagа wanachanganya na



Agnes Daniel; ana mazito ya kuuguza na kupoteza.. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

majivu, wanampa mgonjwa anatumia mwezi wa kwanza mwezi wa pili atapona, kwa sababu anatumia dawa za TB palepale. Lakini mganga wa kienyeji ambaye haibi dawa za TB na kwenda kumtibu mgonjwa, hawezi kupona."

**UBIA NA WAGANGA**

Mratibu wa Kifua Kikuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Dk. Bruno Cronely, anataja changamoto yao ni hiyo imani potofu. Anaendelea: "Katika kutatua hilo, sasa tunafanya kazi na waganga wa jadi au wataalamu wa tiba asili.

"Tumeshawaita, tumewafundisha tumefanya vikao nao pamoja, tumewekeana mikakati na mipango kazi ya kuweza kuboresha huduma ya kifua kikuu katika maeneo yao ya kazi.

"Wanatuonyesha ushirikiano na wameweza kututumia wagonjwa kutoka katika sehemu zao za kazi na tukawaanzishia matibabu na kuna baadhi ya waganga wa jadi na wenyewe wameugua kifua kikuu na wamepata matibabu na wamepona," anafafanua.

Anasema kuna matukio, familia moja ina wagonjwa kati ya wawili hadi wanne, katika dalili zinazofanana na bado wanawapeleka kwa waganga wa jadi na ndio maana tunapeleka katika jamii timu ya watoa elimu.

Anasimulia mwaka jana walipewa lengo la kuibua wagonjwa wa kifua kikuu 340, na wamefanikiwa kuibua wagonjwa 435, sawa na asilimia 127 na mwaka uliopo lengo ni kuibua wagonjwa 500. Hadi Juni iliyopita walishafikisha wastani wa nusu, ikiwapo matarajio kufikisha lengo.

Nini siri ya mafanikio? Bruno anaanika: " Ni kuhamasisha uchunguzi wa kifua kikuu ngazi ya jamii, maana tukikaa kuwasubiri wagonjwa waje hospitali, wapo wagonjwa wengi wanabaki majumbani."

"Yaani anakohoa wiki ya kwanza wiki ya pili anakwenda kwenye duka la dawa au kwa mganga bila kuja hospitali..." anafafanua Dk. Bruno, akitaja mbinu nyingine ya kuwafundisha stadi za ziada watoa huduma kugundua wagonjwa.

Pia, anataja mapungufu katika maabara za vituo vya afya, sio zote zenye uwezo wa kuchunguza TB, sambamba na kuwepo bajeti finyu, akisema:"Inatakiwa tuwe na vitu vingi vinavyo pima na kugundua TB, lakini kwa sasa vipo vitano tu kati ya vituo vyetu 25 tulivyo navyo sawa na asilimia 20."

Vivyo hivyo, anataja katika vituo binafsi, kwamba bado wanaona ukakasi kutibu bure mgonjwa wa TB.

**WANENAVYO WAGANGA**

David Musanganzira ni mganga wa asili anayekiri kwa Nipashe huwa anapokea wagonjwa wa TB na kuna kipindi wanaitwa kwenye semina za kuwaelewesha wagonjwa wa TB na dalili zao.

"Baada ya kusikiliza maelezo yao cha kwanza tunawapa ushauri kwamba waende hospitali wakafanye uchunguzi na baada ya kufanya uchunguzi wanakupigia simu tena.

"Wagonjwa wengi wananifikia kwa sababu mimi ni mganga wa tiba asili ninaetambulika kiserikali na miongoni mwa wagonjwa walionifikia wapo ambao nimewatibu mimi walioniletea kibali cha kunidhirishia kuwa hii ni TB kutoka hospitali," anaeleza.

"Akidhihirisha hivyo, akirudi kwangu namuanzishia dozi maana dozi yangu mimi ni kuanzia miezi mitatu hadi miezi sita. Mimi naifahamu TB sababu, tumekua tukiitwa kwenye semina za madokta ambao wako serikalini wanatuambia ukiona mtu ana dalili hizi ujue hiyo ni TB.

"Dokta Bruno anajua nikweli kabisa nimekuwa nikimpelekea wagonjwa wa TB wengi tu, hawana idadi kwa sababu nilikua siandiki idadi yao, ila ninapomuona mtu mwenye dalili zile nimekuwa mwepesi wa kumpigia simu, anakuja kuwapokea na wengine wanaenda wenyewe,'anaeleza.

"Mimi sipigi ramli kwanza, hata mazingira hayaruhusu kumtambua mtu huyu anaumwa hiki kwanza, lazima uwe na 'kaelimu' kadogo kwamba uitambue baioloji,utambue mwili wa mtu anapotoa 'statement' (taarifa) na wewe utumie experience (uzoefu" kwamba atakuwa na tatizo fulani.")

Anasimulia, wapo wenye tabia chafu, ikiwemo kutaka uhusiano wa kimapenzi na wagonjwa, akiwakosoa waganga jadi wenzake: "Hakuna dawa ya mtu akudanganye kuwa ukienda na mwanamke kule ukifanya naye tendo la ndoa ndio unamtibu hapana, kwanza huo ni udhalilishaji mbaya... watu hao tunawatafuta hata sisi."

**TB INAVYO GOMBANISHA FAMILIA.**

Roza Gilbert (22), mama wa mtoto wa mwaka mmoja na miezi tisa, anasimulia jinsi mwanawe alivyopata kifua kikuu, hatimaye kuleta vurugu ndani ya nyumba na ndoa kuvunjika.

Anasema, hali ya mwanawe ilianza kubadilika alipofikisha umri wa mwezi mmoja, akiona mabadiliko, huku anazidi kudhoofika kiafya, ikawa chanzo cha ugomvi kwenye nyumba yao.

"Mama mkwe wangu akabidi aanze kumshauri mtoto wake ambaye ni mume wangu, kuwa mimi nafanya mambo ya ajabu, natoka nje ya ndoa yangu.

"Sasa siku moja alikuja shangazi akaniambia mama Asia afya ya mtoto wako unaionaje? Mimi nilimwambia unavyoona wewe na mimi ndivyo ninavyoona. Akaniambia itabidi nikupeleke kuna mtaalamu amekuja ambao ndio huyo mganga sasa nikamwambia sawa.

Roza anaeleza baada ya kulipa Sh. 2,000 za ramli, akaambiwa mtoto ana tatizo la ugonjwa uitwao Nsuko, mtoto anakosa vinyweleo na 'Makile' ukihusishwa na mama au baba kutoka nje ya ndoa.

Anasema baada ya kulipa Sh.50, 000 za matibabu ya wiki mbili, pasipo mafaniko akiwa na dawa za kumuogesha, kumnywesha, kumchanja na kumkanda mtoto, hali iko vilevile akaenda kwa mganga mwingine wa kiume.

"Kweli nilifika nikaonana naye, nikatoa hela ya kupigia ramli kama kawaida Sh.2,000 na yeye akaniambia hivyo hivyo kwamba ana Nsuko na Makile gharama ya matibabu ilikuwa Sh.150,000," anasema.

"Basi akaanza kunitibu, akaniambia... mimi nimekupenda, nataka nikuoe. Nikamwambia mimi kuolewa siko tayari, kwanza nina mume wangu, hali ya kuwa tayari nimeshatoka kwangu.

"Akasema hapana mimi nilishajua kila kitu na ninaona kwa sasa haupo na mume wako, ulishatoka kwako. Nikamwambia haijalishi, ila mimi siko tayari kuolewa kwa kipindi hiki. Bado napambana kwanza na usalama wa mwanangu," anasimulia.

Anasema, tabibu huyo akampa vitisho 'nitakachokufanyia nitajua mwenyewe' kipindi hicho mtoto akiwa katika 'dozi' ya kunywesha na kumchanja.

Roza anasimulia kwamba, akahamia kwa mganga wa tatu, alikotozwa Sh. 200,000 alipokwama mtoto kupona, akahamia kwa mganga wa nne aliyemtoza Sh.80,000 za tiba.

"Yeye aliniambia kuna mtu aliementendea hayo kwamba amemloga, aaah! Basi mimi hapo akili nikachanganyikiwa, nikasema yaani huyu tutatambuana vizuri hawezi kunifanyia hivi kwa mwanangu," anaeleza,nayo matibabu hayakufanikiwa.

Mama huyo anasema, akahamia mganga wa tano na mwanamama, ambaye akamuambia aliyefanya hivyo kwa mwanangu ni ndugu wa karibu, akimtoza Sh. 50,000 akimuambia anamuonea huruma ameishiwa, nako hakukuwepo mafanikio ya tiba.

"Sikuchoka, nikaenda kwa mwingine ambaye alikuwa wa sita na yeye alikuwa ni mwanamke. Nimefika pale,



David Musanganzira, mganga wa jadi.



Dk. Bruno Cronely, Mratibu wa Kifua Kikuu



Roza Gilbert; alihangaika kuuguza 'kichanga'

tukawa tumeongeza nikatoa hiyo hela ya ramli Sh.2,000 akaniambia na yeye kama walivyoniambia wale wengine kuwa matatizo ya mtoto wangu amet-endewa na ndugu.

"Wakati naendelea na matibabu pale, kuna nesi mmoja akawa amenishauri baada ya kuona na yeye afya ya mtoto inamchanganya, akasema twende nikupeleke pale St. Mary(hospitali) ukaonane na daktari, amchunguze atoweza kumsaidia.

Anaikumbuka ilikuwa Ijumaa ya Machi 3 mwaka huu, baada ya kukutana na mtaalamu, akamchunguza mtoto,hata akatambua anasumbuliwa na kifua, akamtaka arejee naye siku nne baadaye, Jumanne aanze kupewa dawa.

"Akamfungulia faili, nikaja nikawa nimeanza kumpa kila siku nampa nusu kwa yule mganga wa sita, nikawa nimesitisha kwanza," anasimulia.

Mama Asia anasema, kwa sasa afya ya mtoto wake inaendelea vizuri, amechangamka, uzito umeongezeka wakati anapohojiwa na Nipashe zaidi ya mwezi mmoja sasa, amefika kilo tisa, kutoka kilo saba alipoanza kutumia dawa ya tiba ya kifua kikuu.

Anasema, katika miezi mitatu toka aanze kumpa dozi mwanawe, akiwa katika dira ya matarajio ikifika miezi sita atakoma na mtoto wake atakuwa na kuanza kutembea kama watoto wengine.

Kuhusu ndoa yao, anasema tangu mtoto aanze kuugua, mume wake aliyeshauriwa na mama yake kuwa mke wake anatoka nje ya ndoa na inatakiwa waachane nae, hawajaonana na hajashiriki chochote katika matibabu ya mtoto na hawana mawasiliano

**KINACHOENDELEA MPANDA**

Mratibu wa Kifua Kikuu Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Dk. Bruno Cronely, anaeleza: "Kwa manispaa yetu ya Mpanda ni asilimia 20 pekee ya vituo vya afya vinavyotoa huduma hiyo. Hii ni kutokana na uhaba wa watumishi lakini pia vituo.

"Pia, kuna ufinyu wa vipimo vya vinasaba vinavyopima mdudu wa kifua kikuu yani mashine ambayo inapima kwa usahihi mdudu wa kifua kikuu na inaweza kugundua kifua kikuu hata kama ni kwa kiwango kidogo.

Anasema, Manispaa ya Mpanda inaendelea kujenga maabara katika vituo vyake vya afya ikitegemewa inapofikia mwaka 2023, itakuwa imekamilika, wataalamu wa maabara wataongezwa wa kutosha na kuongezwa vituo vitano mpaka 10.

"Kwa Manispaa yetu ya Mpanda, makundi ambayo yanaathiriwa na kifua kikuu kwa asilimia kubwa ni watu ambao kinga yao ya mwili iko chini, watu wanaoishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kuna watoto walioꞏchini ya miaka 15 na wazee.

"Makundi ya wanaofanya kazi migodini japokuwa sio kwa kiasi kikubwa kulingana na takwimu tulizo nazo na Manispaa yetu Mpanda tunaona kati ya umri wa miaka 35- 44 ndio umri ambao wameathirika zaidi kwa ripoti za mwaka jana 2021,"anasema.

Anataja kundi la vijana linaathiriwa zaidi, kwa sababu ya shughuli zao kijamii na wanaume wanakutana kwenye vibanda vya mpira, vilabu vya pombe na utafutaji ambako kuna msongamano wa watu kama vile kwenye uchimbaji wa madini na viwanda vilivyopo kama vya mpunga.

Dk, Bruno anasema, walio wengi wanachelewa kufika katika vituo vya kutoa huduma za afya, ikilinganishwa na kinamama na kuchangia waambukizane kwa wingi.

"Tuna mipango mingi ambayo tunaendelea nayo ikiwa ni pamoja na kuwafuata katika maeneo yao ya makazi," anaeleza, pia akiahidi usimamizi elekezi katika vituo vya kutoa huduma za afya na kuboresha huduma zilizopo.

"Kundi ambalo linasumbua sana ni vijana kwa sababu dawa za TB ni za muda mrefu mtu atakunywa dawa kwa miezi sita kama ni TB ambayo sio sugu kwa hiyo kile kitendo cha kunywa dawa kwa miezi sita wanaona kama ni kero kwao.

"Mwingine akisha kunywa dawa mwezi mmoja anapoteza matibabu anakuwa mtoro, tunaanza kumtafuta. Pia, kuna kundi la wazee tunaamini wazee kinga yao imeshuka, japokuwa sio wote...unakuta hawaendelei na matibabu, ila tunaendelea kuwatafuta.

"Kwa kupitia mdau wetu Amref ambaye anafanya kazi ya TB ngazi ya jamii na kuwarudisha kwenye matibabu wavivu wanapata dawa vizuri. Naona walio wengi wameishazoea dawa za muda mrefu, kwa hiyo kunywa dawa za TB kwa miezi sita sio changamoto kwao.

"Kwa hiyo hayo ndio makundi yanayo tusumbua sana katika kuendeleza matibabu ya TB hasa vijana ndio wanasumbua sana,"anasimulia.

Anataja timu yao ya kazi inajumuisha kuanzia ngazi ya mkoa, halmashauri, waganga wafawidhi wa vituo vyote, pia watu mashuhuri kwa maana ya viongozi wa dini, watoa huduma vituoni na ngazi za jamii mtaani.

"Watendaji wa kata, watendaji wa mitaa wenyeviti tumeisha waita tumewafundisha lengo nikwamba kila mtu aibebe hii mada," anasema na kuhitimisha:

"Ni kweli kifua kikuu kipo toka zamani, lakini kila mwaka ugonjwa huu umekuwa ukiongezeka kasi. Tunaposema wagonjwa wanaongezeka, hatumaanishi kwamba zamani hawakuwepo, isipokuwa ni njia mbalimbali zinazotumika katika kuibua wagonjwa katika jamii.

**MTIHANI WA KUUGUZA**

Agnes Daniel, aliyepoteza mume Machi 2022 kutokana na ugonjwa kifua kikuu, anasema amehangaika na mumewe sehemu mbalimbali kwa matibabu hadi umauti ulipomkuta.

"Mume wangu alianza kuugua mwaka 2019 nimehangaika nae mpaka 2020, tumeenda Ikonda (Iringa), kupata matibabu mara mbili, tumerudi hapa, tukaambiwa tuende Dodoma, tumeenda napo akafanyiwa matibabu, baada ya kupima wakagundua kuwa ana TB ya matezi.

"Alikuwa ana uvimbe sehemu ya shingo, akafanyiwa opaesheni na kupatiwa dawa za kumeza, basi tukawa tumerudi. Baada ya kufika, aliendelea kumeza dawa kama miezi sita, nikajua sasa hapa labda tayari Mungu atasaidia pakawa panaonyesha kupungua, lakini baada ya kufika mwezi wa saba, akavimba tena sana tofauti na mwanzo!

"Ikabidi twende hospital ya hapa, Mpanda kufika tukaambiwa inatakiwa turudi Dodoma, alikotibiwa sasa hali yenyewe ya maisha ilivyokua ikabidi nirudi tu nyumbani tukakaa kwanza.

"Basi wakawa wametokea wahudumu wa Kituo cha Afya Mwangaza, wakaniambia hiyo ya miezi sita uliotibu ilikuwa ni TB ya mapafu, kumbe kuna dawa za kumeza mwaka mzima.

"Basi mimi nikawa nimeanza tena kufuatilia hizo dawa akawa ameanza kumeza ilipofika muda wa mwezi mmoja akaanza kuonyesha kujaa miguu, mara tumbo, chakula hali, nikaenda kuwaambia wakasema hiyo ni hali ya hivyo vidonge anavyomeza nikasema sawa nikarudi.

"Hali iliendelea kuwa mbaya nikaenda Hospital ya Mpanda kupima wakakuta mapafu... mwisho wa siku umauti ukawa umemkuta," anasimulia.

Anaeleza ni ugonjwa uliochukua uhai wa watu sawa katika familia ya mumewe, wajomba watano na mama zake wawili.

Nipashe ililihamia familia ya Jenifer Patrick, ugonjwa uliowapata wanawe wawili, kwa nyakati tofauti, akianza na wa kiume akisumbuliwa na homa na muda mrefu analala tu, baada ya uchunguzi hospitalini ikagundulika kifua kikuu.

Agnes anadems, akaambiwa mgonjwa anapaswa kwenda kutibiwa Moshi, akifafanua mkasa: "Wiki ya kwanza ikaisha, ya pili ya tatu, ndio anakuja kuleta majibu wakapiga simu wakasema kesho ndio watamwijia, kama jana yake tulikuwa tumesha mzika."

Anadems, baada ya muda mfupi na bintiye naye akaanza kuugua homa, waliporejea hospitalini na wakasema ana shida ya kifua naye anatakiwa akatibiwe Moshi, alikohudumu huko wastani wa miaka miwili.

Wakati anaondoka mgonjwa alikuwa kafaulu kuendelea na sekondari na aliporejea, akawakuta wenzake wako kidato cha pili, akakataa kuendelea na masomo kwamba ameshachelewa.

"Siku mimi sipo wakaniambia 'mtoto wako anarudi', nikasema 'anarudi?' wakasema eee! mara anakuja kumuona huyu hapa kapona kabisaa!" anaeleza.

AFYA

# Maradhi ya akili yalivyofika mbali, kila mmoja sasa ni wa kujitathmini

- Kula kupita kiasi, wivu nao ukizidi...
- Mkoa Mbeya uko juu unatikisa kitaifa

**Na Yasmine Protace**

MAGONJWA ya afya ya akili, ni sehemu ya matatizo ya ubongo yanayomfanya mtu kuwa na hasira,fikra na matendo tofauti na uhalisia wa kibinadamu, hata jamii yake na kumsababisha kushindwa kukabiliana na changamoto za kimaisha.

Inaelezwa, magonjwa ya afya ya akili, yanaweza kusababishwa na sababu za ama kibaiolojia au kisaikolojia, kwani afya ya akili inajumuisha pamoja na matendo ya ustawi wa akili, mihemko, kisaikolojia na kijamii.

Afya ya akili inaathiri jinsi mtu anavyofikiria, kuhisi na kutenda. Mkurugenzi wa Mawasiliano kutoka taasisi isiyo ya kiserikali, Jukwaa la Kupambana Kuzuia Tabia za Watu Kujiua Tanzania (TSPC), Mayasa Kalinga , anasema kuwa wivu kupita kiasi kwa wanandoa na wapenzi wao, ni hali inayochangia watu kupata tatizo la afya ya akili na kusababisha kufanya matukio ya kikatili.

Mayasa anasema katika mada yake inayohusu wimbi la ukatili kwa wanandoa na wapenzi, ana ufafanuzi kwamba: "Wivu kupita kiasi kwa wanandoa na wapenzi husababisha watu kupata ugonjwa wa afya ya akili."

Anaongeza kuwa unyanyasaji, ubaguzi na ukiukwaji haki za binadamu kwa wanawake, vimekuwa kichocheo katika kudorora afya ya akili kwa wanawake.

Mayasa anasema takwimu za Jeshi la Polisi kuanzia Januari mwaka jana hadi Juni 2021 zinaonyesha jumla ya watu 15,131 walifanyiwa ukatili wa kijinsia na kuna ongezeko la mauaji kwa wanawake walio katika ndoa.

Hapa ana ufafanuzi kwamba, matukio ya mauaji na ukatili wa kijinsia hasa kwa wanandoa yameendelea kuongezeka nchini, hali iliyoibua sintofahamu kuhusu usalama wa hali ya afya ya akili na usimamizi wake kitaifa.

Anaeleza kuwa ripoti ya mwaka mwaka jana, mwezi kama huu (Septemba) iliyotolewa na Jarida la Afrika kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia, Tanzania ni miongoni mwa mahali paliko wanandoa hufanyiwa ukatili mkubwa wa kijinsia.

"Asilimia 46 ya wanandoa hufanyiwa ukatili wa kijinsia; asilimia 36 walifanyiwa ukatili wa kimwili; asilimia 32 walifanyiwa ukatili wa kisaikolojia; na asilimia 13 walifanyiwa ukatili wa kingono," anafafanua mtaalamu huyo.

Mayasa anaeleza kuwa katika ripoti ya Shirika la Afya Duniani ya mwaka 2001-2002, inaonyesha kuwa nchini katika mkoa wa Mbeya wanawake, waliofanyiwa ukatili wa kijinsia kwa jumla yao ni 1820, mbao ni sawa na asilimia 87.

Pia, ukatili huo kwa mkoa wa Dar es Salaam, kuna wanawake walifanyiwa ukatili ya kijinsia jumla yao ni asilimia 41.

Anasema utafiti wa mwaka 2020, nao unaonyesha jumla ya watu bilioni moja duniani wanaishi na magonjwa ya afya ya akili na saba inatokana na matukio ya kikatili, kutokea kila mara.

Katika hilo, Mayasa anaomba elimu ya afya ya akili ianze kutolewa, ikianza na ngazi ya shule za msingi na kupanda sekondari, hadi vyuoni na katika hilo anashauri serikali iongeze bajeti kubwa katika afya ya akili kutokana na kutengwa kwa bajeti ndogo ya Afya ya akili.

" Kwa kuwa ugonjwa upo kwa jamii,serikali inatakiwa iongeze bajeti hiyo,kiasi cha shilingi bilioni mbili kilichotengwa kwa ajili ya afya ya akili ni kidogo kutokana na tatizo kuwa kubwa," anasema.

Anafafanua athari zitokanazo na ukatili wa kijinsia kati ya wanandoa na wapenzi wao ni moja ya kusababisha msongo wa mawazo, matatizo ya dawa za kulevya, kula kupitiliza na tabia ya kufanya ngono hatarishi.

Mayasa anaeleza kuwa, kati ya watu wanne nchini, mmoja ana tatizo la afya ya akili na

asilimia 75 ya watu wenye matatizo ya akili hawapati matibabu.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya jinsia na maendeleo ( DSS), wakisikiliza mada ya afya ya akili, iliyoandaliwa na Jukwaa la Kuzuia Watu Kujiua Tanzania ( TSPC). **PICHA: YASMIN PROTACE.**

### SHIDA NINI?

Zahara Omary, ni mshiriki wa GDSS kutoka Kivule, Dar es Salaam, anasema hali ya watu kuishi kwa mazoea katika ndoa, inachangia sana ukatili wa kijinsia.

Anasema, kutokana na kuwa mwanaharakati katika masuala ya kijamii, ameshuhudia changamoto za wanandoa au wapenzi wanavyozifanya kama mazoea.

" Huku Kivule kuna familia ambayo hata majirani waliiona kama kawaida kwa wanandoa, mwanandoa mwanaume kujisaidia kila siku chumbani na kuonekana ni kitu cha kawaida," anasema.

Anasema wanandoa hao hugombana na kusababisha mwanamke kukimbia nyumba akiwaacha watoto na baada ya hatua hiyo, watoto walifungiwa hadi jamii ilipogundua kasoro na kuingilia kati, watoto hao wakiwa wameshaathirika kisaikolojia, hata kiafya.

Hassan Juma, mshiriki wa GDSS, anasema kuwa inafaa elimu itolewe ya afya ya akili kuanzia elimu ya msingi hadi vyuoni.

Anasema viongozi wa dini na hata wasanii wanapaswa kuwaelimisha wanajamii athari zitokanazo na magonjwa ya akili.

" Viongozi wa dini na wasanii wanakuwa na watu wengi ambao wanawasikiliza,hivyo watumie nafasi hiyo kuelimisha jamii juu ya ugonjwa wa afya ya akili,"anasema.

Anasema kutokana na bajeti ndogo ya magonjwa ya afya ya kutengwa na serikali, kunatakiwa kuongozwe hatua za kusaidia jamii isiathirike na magonjwa ya afya ya akili.

Mariam Jamili mshiriki wa GDSS, anasema asilimia mbili iliyotengwa katika bajeti ya afya ya akili ni ndogo.

Anasema baadhi ya makabila kuna vitu wanaviendekeza na kusababisha kuchangia masuala ya afya ya akili, akiitaka

serikali iendelee kutoa elimu ya ziada kuhusu afya ya akili, ili jamii iendelee kuutambua ugonjwa huo na wachukue hatua.

Mariam anasema kwamba serikali na mamlaka nyinginezo zichukulie hatua stahiki, pia serikali kwa kuongeza nguvu zaidi katika kupambana na afya ya akili .



Mtu anayesadikiwa kuwa na shida ya afya ya akili. **PICHA: MTANDAO.**





## CSSC kuwezesha vituo vya afya vya makanisa kujiendesha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TUME ya Kikristo ya Huduma za Kijamii (CSSC), kupitia mradi wa pamoja Tuwekeze Afya, imejipanga kuwezesha vituo vya afya vya makanisa kujiimarisha na kujiendesha kwa mapato ya ndani bila kutegemea ufadhili kutoka nje.

Meneja wa mradi huo, Dk. Godfrey Kway, aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa 85 wa Chama cha Madaktari wa Hospitali za Mashirika ya Dini (TCMA), uliofanyika jijini hapo.

Alisema mradi huo umeleta mafanikio mbalimbali ikiwamo kuongeza wateja kwa asilimia 22 pamoja na kuongeza mapato ya hospitali kwa wastani wa asilimia 34 kwa mwezi.

"Mradi huu unalenga kuimarisha vituo vya makanisa ili kujitegemea kifedha na kupitia mradi huu vituo vya afya 11 vimefikiwa hadi sasa na vinatoa huduma bora kwa wananchi katika maeneo ya vijijini," alisema.

Alieleza kuwa vituo vyao vimekuwa vikitegemea ufadhili na fedha kutoka nje ambapo kwasasa umepungua na vimeanza kuyumba.

"Tuliona kama kanisa tuje na mradi huu ili kuvisaidia vituo hivi kuongeza ubora na mapato na kutengeneza huduma zao pamoja na kuboresha huduma za uongozi ili kuwavutia wagonjwa na pamoja na kutatua changamoto ya kukosekana kwa dawa."

"Mpaka sasa tumeanza kupata mafanikio makubwa cha kwanza ilikuwa kutoa uelewa kwa viongozi wetu wa dini. Vituo vimeanza kupata mafanikio makubwa hasa kwenye bima kwani mapato ya mwezi yameongezeka maradufu ndani ya mwaka," alisema Dk. Kway.

Kwa upande wake, Dk. Ringo Mtei wa Tume hiyo, alisema jukumu lao kubwa ni kuhakikisha vituo hivyo vya afya vya kanisa vinatoa huduma bora kwa wananchi.

"Changamoto ilikuwa ni vituo haviwezi kujiendesha vingine hata kulipa mishahara ilikuwa ni shida na hata dawa zilikuwa hazipatikani na vituo tulikuwa tukiwategemea wahisani," alisema.

Naye Mganga Mfawidhi kutoka Hospitali Teule ya St. Joseph Moshi, Sista Dk. Hellen Kyilosudu, alisema wamepata mafunzo mbalimbali ya namna ya kuendesha hospitali kwa faida na kupitia mafunzo hayo mafanikio makubwa yameonekana.

Alisema wanahakikisha wanatoa huduma bora kwa wagonjwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanaondokana na uhaba wa dawa, wafanyakazi wote kufuata miongozo na kujiwekea malengo na kutunza kumbukumbu zao vizuri ili kuepukana na upotevu wa mapato unaotokea katika maeneo mbalimbali.

# TBA yashauriwa kuongeza ujenzi nyumba za watumishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BUNGE limeshauri Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza uwezo wa kujenga nyumba nyingi zitakazosaidia kupunguza uhaba ulipo kwa watumishi wa umma badala ya kuendelea kutegemea ruzuku ya serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji Mitaji ya Umma (PIC), Jerry Silaa, alitoa ushauri jana jijini hapo baada ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa miradi mbalimbali unaotekelezwa na TBA.

Kamati hiyo ilitembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Shirika la Umeme nchini (TANESCO), ujenzi wa nyumba 20 za viongozi Kisasa pamoja na mradi wa ujenzi wa nyumba 150 za watumishi eneo la Nzuguni.

Akizungumza katika ziara hiyo, Silaa alisema hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, aliushauri wakala huo kutafuta namna ya kuanza kufanya biashara ili kukidhi mahitaji makubwa ya nyumba kwa watumishi yaliyoko hivi sasa.

"Agosti 31, mwaka huu, kamati yetu ilikutana na TBA na leo hii tulikubaliana kuja kutembelea miradi ambayo wanaitekeleza na kamati imeridhishwa na utekelezaji wa miradi yote."

"Kama ambavyo Rais alitoa ushauri kwa TBA pia sisi Bunge tunaishauri TBA kuona namna ambavyo inaweza kufanya kazi kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza uwezo wake wa kujenga nyumba kwa wingi ili kukabili uhaba uliopo hivi sasa badala ya kuendelea kutegemea ruzuku kutoka serikalini," alisema.

Alisema, kamati hiyo inashauri taasisi zingine kama Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na TANESCO, kupeleka miundombinu katika maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa.

Mtendaji Mkuu wa TBA, Daudi Kondoro, alisema tayari ameshaanza makubaliano na baadhi ya sekta binafsi ikiwamo ujenzi wa duka kubwa (Mall) eneo la Magomeni Dar es Saalam na nyumba ya makazi ya ghorofa moja eneo la Mikocheni.

"Lakini tutaendelea kutekeleza ujenzi wa miradi yetu kwa kujenga maghorofa ili kuwa na matumizi bora ya ardhi," alisema.

Akizungumzia miradi iliyokaguliwa na kamati hiyo ya Bunge, Kondoro alisema ujenzi wa makao makuu ya TANESCO wameshiriki na ubunifu walifanya watu wengine.

Alisema katika ujenzi wa nyumba za watumishi Nzunguni jijini Dodoma wamepanga kujenga nyumba 3,500 na wameanza na nyumba 150 ambazo zitakamilika Desemba, mwaka huu.

"Oktoba mwaka huu tunapanga kuwa tumekamilisha nyumba 50, Novemba pia 50 na zingine 50 za mwisho tunapanga kuzikamilisha ifikapo Desemba mwaka huu," alisema.

Hata hivyo, alisema hadi sasa katika ofisi yao ya mkoa wameshapokea maombi ya watumishi 900, ambao wanahitaji nyumba kwa ajili ya makazi.



Makamu Mkuu wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dk. Michael Msendekwa, akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya siku tano kwa viongozi wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa (ALAT) kutoka Mkoa wa Mwanza, yaliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Halmashauri zakumbushwa kukitumia Chuo Hombolo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

HALMASHAURI za Serikali za Mitaa nchini zimetakiwa kukitumia Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kujiimarisha kwenye masuala ya serikali za mitaa.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Michael Msendekwa, aliyasema hayo alipokuwa akifunga mafunzo kwa viongozi wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa (ALAT), Mkoa wa Mwanza yaliyofanyika jijini hapo.

Alizitaka halmashauri zote nchini kukitumia chuo hicho kwa sababu kilianzishwa kwa ajili ya kufundisha masuala yanayohusu serikali za mitaa.

"Naomba nitoe wito kwa halmashauri zingine zote nchini, hiki ndiyo chuo chao, ndicho chuo kinachofundisha masuala ya serikali za mitaa, hivyo wanakaribishwa kukitumia wakati wowote," alisema.

Aliyataja baadhi ya mafunzo yanayotolewa na chuo hicho kuwa ni uongozi na utawala bora, sheria za uendeshaji wa serikali za mitaa na usimamizi wa mapato na matumizi pamoja na ubunifu wa uanzishwaji wa mbinu mpya za kuongeza mapato kwenye halmashauri husika.

Kadhalika, aliyataja mafunzo mengine yanayotolewa chuoni hapo kuwa ni usimamizi wa watumishi wa katika halmashauri za serikali za mitaa na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na manunuzi.

Dk. Msendekwa alisema wamekuwa wakifanya mafunzo kwa njia ya ana kwa ana pamoja na matumizi ya njia ya kielektroniki ambayo hufundishwa kwa njia mtandao.

Pia alisema mafunzo ya mara kwa mara yanasaidia kubadilishana uzoefu wa kuwahudumia wananchi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Naye Mjumbe wa ALAT Mkoa wa Mwanza, Anifa Mwita, alisema wanatarajia kupata mafunzo namna ya kusaidia kusimamia vizuri mapato ya halmashauri yanayokusanywa kwenye maeneo yao.

Alisisitiza kuwa mafunzo hayo yatawasaidia kusimamia fedha zinazotolewa na Serikali Kuu kwenye miradi ya elimu na afya ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Mwanza, Mpandule Simon, alisema waliamua kwenda chuoni hapo kwa lengo la kujengewa mafunzo wa uongozi katika maeneo yao ya kazi.

Alisema katika msafara huo kuna wajumbe zaidi ya 35 kutoka Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Manispaa ya Ilemela na Halmashauri za Magu, Misungwi, Sengerema Buchosa na Ukerewe.





# Ushirikiano Tanzania, Malawi waanza kuzaa matunda mpakani

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

USHIRIKIANO wa majeshi ya Tanzania na Malawi katika kudhibiti uhalifu unaovuka mipaka, umeanza kuzaa matunda baada ya kuwakamata vijana watatu walioiba gari jijini Mbeya na kwenda kuliuza nchini Malawi.

Hivi karibuni aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Malawi, Dk. George Kainja na aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, walifanya kikao cha pamoja jijini hapo na kukubaliana kushirikiana katika mambo mbalimbali ikiwamo kudhibiti wahalifu wanaovuka mipaka.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema gari lililokuwa limeibwa ni aina ya Toyota Prado lenye namba za Usajili T. 795 DEX.

Alisema gari hilo mali ya Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda (45), liliibwa Aprili 4, mwaka huu saa 02:00 usiku katika eneo la Jelele, Kata ya Itezi jijini hapo.

Alisema baada ya mmiliki wa gari hilo kutoa taarifa ya kupotelewa na gari hilo, makachero wa jeshi hilo walisambaa katika maeneo tofauti kwa ajili ya kulitafuta, lakini hawakulipata.

Alisema waliendelea na upelelezi ambao ulisababisha kunaswa kwa watuhumiwa watatu, Yusuph Ramadhani (26), Shuku Nyema, mkazi wa Soweto (23), mkazi wa Songea mkoani Ruvuma na Abuu Rutagalama (26), mkazi wa Itezi.

Alieleza kuwa katika mahojiano, watuhumiwa walikiri kuhusika na wizi huo na kuwa gari hilo wamelisafirisha hadi nchi ya jirani ya Malawi na kumkabidhi Richard Ng'oma raia wa Malawi.

Kupitia ushirikiano wa ujirani mwema baina ya nchi ya Malawi na Tanzania, Agosti 31 mwaka huu hadi Septemba 2, Jeshi la Polisi mkoani Mbeya lilifika nchini Malawi na kushirikiana na polisi wa nchi hiyo ambao walifanya ufuatiliaji na kumkamata Ng'oma akiwa na gari hilo na kukiri kulipokea kutoka kwa mtuhumiwa Yusuph Ramadhan.

"Baada ya Ng'oma kukutwa na mali hiyo ya wizi, Septemba 2, alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kalonga nchini Malawi na kutolewa ushahidi na mmiliki wa gari hilo, Gidion Mapunda na mtuhumiwa Yusuph Ramadhani ambapo baada ya mahakama kujiridhisha na ushahidi uliotolewa ilimtia hatiani mtuhumiwa," alisema Kamanda Matei.

"Baada ya taratibu kukamilika tulikabidhiwa gari hilo pamoja na watuhumiwa kwa ajili ya taratibu za kumjereshea mmiliki wa mali hiyo," aliongeza Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei amewataka wananchi kusalimisha silaha haramu kwa hiari zinazomilikiwa kinyume cha sheria kwa kuhakikisha wanapeleka kwenye ofisi za serikali za mtaa au serikali kuanzia Septemba mosi hadi Oktoba 31, mwaka huu.

Alisema baada ya kipindi hicho polisi itafanya operesheni maalum kichwa kwa kichwa, nyumba kwa nyumba ili kuwabaini na kuwachukulia hatua za kisheria watakaobainika kukaidi agizo hilo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akiwaonyesha waandishi wa habari mkoani humo juzi, sehemu ya tani 20 za bangi iliyokamatwa wilayani Chunya kutoka kwa mfanyabiashara ambaye alikutwa na misokoto zaidi ya 3,500. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Miradi 45 kufikiwa na Mwenge wa Uhuru

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MIRADI 45 ya maendeleo katika sekta ya afya, maji, barabara na elimu yenye thamani ya Sh. bilioni 14.7 inatarajiwa kufikiwa na mbio za Mwenge wa Uhuru ambao uliingia jana mkoani humo ukitokea mkoani Iringa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alipokea Mwenge huo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, ambaye aliukabidhi Igawa wilayani Mbarali.

Alisema kuwa miradi itakayotembelewa ni pamoja na iliyokamilika, itakayowekewa jiwe la msingi na itakayokaguliwa kujua hatua zilizofikiwa katika ujenzi wake.

Aliwataka watumishi wa wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya kuwa tayari kuupokea Mwenge huo maeneo wanayoishi kwa madai kuwa dhumuni ni kukagua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Mkoa wa Mbeya tayari tulishaupokea Mwenge na tunaendelea na shughuli za ukaguzi na uzinduzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, tunatarajia kutembea kilomita 1,014 kufikia miradi hiyo kwenye halmashauri zote saba za mkoa huo," alisema Homera.

Aidha, aliwaomba wataalamu wote wa halmashauri wanaosimamia miradi ya maendeleo kutoa ushirikiano wakati utapofika ili kujua gharama na thamani ya miradi hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Rueben Mfune, alimhakikishia Homera kuwa wilaya hiyo imekamilisha miradi yote inayohitajika kwa wakati na kwa kuzingatia ubora utaotakiwa.

Mwenge wa Uhuru kitaifa ulianza kutembelea miradi ya maendeleo kwa siku saba mkoani Mbeya kuanzia jana hadi Septemba 13 chini ya kiongozi wake, Sahili Geraruma na kisha kukabidhiwa mkoani Songwe.

# Shule za msingi zapewa vitabu 50,000 Kiingereza na Hisabati

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

ZAIDI ya vitabu 50,000 vya masomo ya Kiingereza na Hisabati vimetolewa na Kampuni ya Bioland International Limited inayojihusisha na ununuzi wa zao la cocoa kupitia mradi wake wa kufadhili elimu ujulikanao kwa jina la Cocoa for Schools kwa shule za msingi zilizoko katika Halmashauri za Busokelo na Rungwe.

Lengo la utoaji wa vitabu hivyo ni kukabiliana na tatizo la uhaba wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia kwa masomo ya Hisabati na Kiingereza.

Mfadhili wa Cocoa for Schools, Fons Maex, jana alisema pia wana lengo la kuongeza ufaulu wa masomo ya Hisabati na Kiingereza kutokana na wanafunzi kufanya vibaya katika masomo hayo.

"Zaidi ya Sh. milioni 30 zimetumika kununua vitabu hivi ya Hisabati na Kiingereza ambavyo naamini vitaongeza ufaulu kwa watoto wetu maana tulibaini miongoni mwa sababu zinazochangia kufanya vibaya kwenye masomo hayo ni uhaba wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia," alisema Maex.

Aliwataka walimu wa shule za msingi katika Halmashauri ya Busokelo na Rungwe kuongeza bidii ya kufundisha watoto ili mitihani ijayo halmashauri hizo ziwe kinara.

Akizungumza wakati wa hafla ya kupokea vitabu hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alitoa onyo kwa walimu wanaopanga kuhamia shule zilizoko mjini.

Alisema walimu waendelea kufundisha kwenye vituo vyao vya kazi na kwamba miongoni mwa mambo yanayoendelea kuboreshwa ni pamoja na kupatiwa vitabu vya kufundishia.

"Nawashukuru sana kampuni ya Biolands International Limited kwa msaada huu wa vitabu kupitia programu yao Cocoa for Schools, mmekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha mazingira ya elimu wilayani Rungwe pamoja na mazingira ya biashara kupitia zao la Cocoa ambalo nyie ndiyo wanunuzi wakubwa," alisema Dk. Anney.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau, alisema licha ya serikali kuboresha miundombinu ya shule ikiwamo vyumba vya madarasa, vyoo na baadhi ya vifaa vya maabara bado kuna uhitaji mkubwa wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia hususani kwenye masomo ya Sayansi.

Alisema kwa sasa mazingira ya mwanafunzi kukaa shuleni yatakuwa mazuri na yatamvutia kwa kuwa atakaa kwenye mazingira safi na kujisomea kwa utulivu ili kutimiza ndoto zake.





Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid (kulia), akizungumza na Balozi wa Cuba nchini, Yordenis Despaigne Vera, aliyefika ofisini kwake, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yabaini kiini shida uhaba wa ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alibainisha hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi alipojibu swali la Mwakilishi wa Kiembe Samaki, Suleiman Haroub, aliyetaka kujua mpango wa serikali kuwasaidia wananchi kunufaika na sekta ya uwekezaji.

Waziri Soraga alisema serikali inachukua jitihada mbalimbali za kupambana na tatizo hilo ikiwamo kuanzisha wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ambao una lengo la kuimarisha sekta ya ujasiriamali kwa kutoa mafunzo, miundombinu ya uwezeshaji, mitaji, mikopo na masoko.

"Hii yote ni kwa sababu ya kukuza ujuzi ili wananchi wetu wazitumie fursa mbalimbali zilizoko katika sekta ya uwekezaji na sekta zingine za uzalishaji kwa sababu kuna vilio vya wawekezaji kuwa vijana wengi wa Zanzibar wanakosa ujuzi unaohitajika katika sehemu za kazi," alifafanua.

Waziri huyo alisema fursa hizo zinawanufaisha vijana wote, hivyo ni vyema kuwahimiza vijana katika majimbo kuzichangamkia fursa hizo na zingine zinazotokea.

Alisema Serikali ya Zanzibar kupitia ofisi yake kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma, binafsi na washirika wa maendeleo (Shirika la Kazi Duniani - ILO) imeandaa na inaendelea kutekeleza programu mbalimbali za kukuza ajira (kujiajiri na kuajirika) kwa vijana.

Waziri Soraga alisema programu hizo ni pamoja na mafunzo kazi na mafunzo ya muda mfupi ya kukuza ujuzi (NEET - Not in Employment, Education or Training).

Alisema programu hizo zinaongeza ujuzi wa vijana kujikita na fani mbalimbali za ajira ili bidhaa zao ziwe na ubora na zitambulike na zikubalike ndani na nje ya nchi.

"Mafunzo haya yatasaidia kupata fursa za ajira kwa vijana katika sekta mbalimbali za uwekezaji na kupata uhusiano mwema katika kazi zao kutokana na kuwa na ujuzi unaohotajika," alisema.

Waziri huyo pia alisema serikali inaendelea kujenga vyuo vya amali ili kuwawezesha vijana kuongeza ujuzi katika fani mbalimbali ili kujiajiri na kuajirika katika sekta mbalimbali nchini.

# Sababu idadi kubwa mahabusu yatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Muhammed, amesema kuwapo kwa idadi kubwa ya mahabusu katika magereza Zanzibar kunatokana na kushindwa kukidhi vigezo vya kupatiwa dhamana watuhumiwa kwa mujibu wa sheria.

Alibainisha hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wanawake, Aza Januar Joseph, aliyetaka kujua mkakati wa serikali kupunguza mrundikano wa mahabusu.

Alisema kuwapo kwa mahabusu wa kesi zisizokuwa na dhamana kisheria zikiwamo kesi za udhalilishaji wa kijinsia, pia kumechangia mrundikano huo.

Waziri huyo alisema kisheria suala la kutoa dhamana kwa mahabusu ambao wapo Chuo cha Mafunzo (Magereza) ni jukumu la mahakama kwa kuzingatia maelekezo ya kisheria.

Alisema Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaendelea kuimarisha ushirikiano na mahakama kupitia vikao mbalimbali kujadili suala la mrundikano wa mahabusu ili kuona namna bora ya kulitafutia ufumbuzi unaofaa.

Waziri huyo alisema serikali kupitia Chuo cha Mafunzo ina mikakati maalum kwa ajili ya kupunguza mrundikano wa mahabusu magerezani.

Alitaja mikakati hiyo kwa upande wa Gereza la Kiinua Miguu mjini Zanzibar ni pamoja na kuendelea kufanya ukarabati mkubwa wa chuo hicho ili kiwe na uwezo wa kutosha wa kuhifadhi mahabusu.

"Pia kuwa na vikao vya pamoja kati ya Chuo cha Mafunzo, Ofisi ya Mahakama, Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuona namna ya kuishauri mahakama kuchukua hatua za haraka ili kukamilisha kesi na kutolewa hukumu kwa wakati," alisema.

Waziri huyo alitaja mkakati mwingine ni kulihimiza Jeshi la Polisi na taasisi nyingine za kiuchunguzi kuharakisha upelelezi ili kesi ziendeshwe kwa haraka na ujenzi wa magereza mapya likiwamo la Hanyegwa Mchana, Mkoa wa Kusini Unguja.

# Sheria mpya tatu zatungwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Wawakilishi Zanzibar limepitisha miswada mitatu ya sheria baada ya sheria hizo kutiwa saini na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na kuwa sheria kamili.

Akizungumza jana katika kikao cha baraza hilo Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar, Spika wa Baraza hilo, Zuberi Ali Maulid, alitaja kuwa ni Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Sh. trilioni 2.59 kutoka Mfuko Mkuu na Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 2023 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Alisema muswada mwingine ni wa sheria ya kutoza kodi na kufuta baadhi ya kodi na tozo na kurekebisha baadhi ya sheria za fedha na kodi zinazohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Alisema muswada wa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake nao umekuwa umepitisha kuwa sheria.

"Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 92(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020, ninaomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo niliyoitaja sasa imekuwa sheria kamili baada ya kutiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi," alisema Spika Zuberi.

Wajumbe wa baraza hilo jana walipitisha muswada wa sheria wa kufuta Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa) No. 4 ya 2007 na kutunga sheria mpya ya baraza hilo katika kutekeleza kazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema sheria hiyo itakapofanyiwa marekebisho itasaidia kupunguza kero za wananchi, kuhimili mgawanyo wa madaraka katika muhimili wa dola, uhuru wa kujieleza pamoja na mahitaji ya watu wenye ulemavu.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 113 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOHN MAKWENYA MUWENA.**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTER ADMINISTRATION BY ELIZABERT SIMON MALAMLA ........... PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn NO.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 3 Day of 10,2022.
**Dated at Dodoma this 6 day of September, 2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA VYETI



**CECILIA ARON MGALA** Anatangaza kupotelewa na **CHETI CHA FORM FOUR(CSEE)** chenye Index Number: **S5137-0003** Kilichotolewa na Baraza la Mtihani la Taifa kupitia shule ya **ST. MONICA CATHOLIC SEMINARY** mwaka **2015** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi
**RB namba DAR/CHA/RB/354664/2022.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**GEOFFSONS ENTERPRINEURSHIP CO LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **SUNLG** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 545 BZT .** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
**TAARIFA YA POLISI**
**KAH /RB/ 591 /2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 177 YA MWAKA 2019**

**HAWA NICHOLOUS GONDWE.......................................MDAI**

**VERSUS**

**AMSABI JEREMIAH MRIMI.................................... MDAIWA**

**KWA: AMSABI JEREMIAH MRIMI**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe tarehe 26.09.2022 saa 3.00 asubuhi.Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** -Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hiloi leo tarehe 06 ya Mwezi wa September,2022.

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO....08....OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GERVAS STEPHANO NKEMBO**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION BY LUCY HERMAN MBELE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be field on or before the 22 day of September 2022
**Dated at Korogwe this 30 day of August 2022**

DISTRICT COURT KOROGWE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **ZAWADI RAMADHANI MNZAVA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISH FUSO** yenye namba za usajili **T. 485 AMS.** Yenye Engine namba **6D16713837** na Chassis namba **FK417E750696.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**TaarifaPolisi: TAN/RB/354433/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH GEORGE MANTANO,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyata Mark II, yenye no za usajili **T534BPV,** ENGINE NO **1j21218806,** CHASSIS NO **jzx1106043130.** Yeyote akaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**DOD/DOD/RB/355035/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMILIANA ERICK LENARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye iindex namba **PS.0203134/087** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya msingi **NAKASANGWE** mwaka **2017**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI CONTROL NAMBA: 9910834214745**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 16 YA MWAKA 2008**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**AMANI KASSIM**
**MWOMBAJI**
**KASSIM AMAN KASSIM**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 28 Mwezi wa 9, 2022.
**Imewasilishwa Dar es salaam leo tarehe 8 Mwezi 9, 2022.**

NAIBU MSAJILI

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**SIMON JOSEPH CHAMY**
Anatangaza kupotelewa kwa passport ya kusafiria yenye namba za usajili **TAE347607** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0757064471. MOR/MOR/RB/354163/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 122 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the late YOHANA JONATHAN MKUMBO of IPAGALA within DODOMA REGION.**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS ADMINISTRATION BY MARY YOHANA MKUMBO**
**PETITION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION WHEN DECEASED DIED INTESTATE**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 of PROBATE RULES GN 369 Of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 Day of 09/2022.
**Date at Dodoma this 21 Day of July, 2022.**

.............................................
**PETITIONER**
**Presented for filing this 2...... day of .........09/ 2022**
.......................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**







**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Ruto, Kenyatta wajadili kukabidhiana uongozi

**NAIROBI,** KENYA

RAIS mteule wa Kenya, William Ruto amefichua kuwa amefanya mazungumzo ya simu na Rais anayemaliza muda wake, Uhuru Kenyatta.

Katika taarifa yake, ilieleza Ruto na Kenyatta walijadili upigaji kura uliyohitimishwa Agosti 9 na mchakato wa mpito kama ilivyoainishwa katika Katiba.

"Nilifanya mazungumzo ya simu na bosi wangu, Rais Uhuru Kenyatta. Tulijadili Uchaguzi Mkuu uliomalizika hivi punde na mpito kama inavyotarajiwa na mila na desturi zetu za kidemokrasia." Alisema Ruto.

Uhusiano kati ya wawili hao ulihar-ibika baada ya Rais Kenyatta kuamua kumuunga mkono Raila Odinga katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi wa Urais 2022.

Wakati wa kampeni za uchaguzi huo wawili hao walirushiana cheche za maneno hadharani kuthibitisha uhusiano wao kuwa mbaya.

Na hata baada ya William Ruto kutangazwa mshindi wa uchaguzi wa mwaka huu na kupewa pongezi kutoka viongozi wa maeneo mbalimbali, Kenyatta hajampongeza naibu wake. **BBC**

## Maporomoko yaua 15 Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

MAPOROMOKO ya ardhi yaliyosababishwa na mvua kubwa yameaua watu 15, wengi wao wakiwa wanawake na watoto katika kijiji cha Kasese, magharibi mwa Uganda.

Katika mkasa huo, baadhi ya nyumba zilisombwa na maji ya mafuriko ambayo yalipitia eneo lililo chini ya milima ya Ruwenzori.

Msemaji wa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Uganda alisema watu sita walijeruhiwa katika maporomoko hayo kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha.

Aidha, Idadi ya watu isiyojulikana inadaiwa wametoweka.

Mkoa huo umekumbwa na maporomoko ya udongo na kushuhudia watu watatu wakifariki wiki iliyopita wilayani Bundibugyo.

Mvua, ambayo kwa kawaida huanza kunyesha mwezi Agosti, mwaka huu imesababisha uharibifu mkubwa katika baadhi ya maeneo ya nchi hiyo.

Mapema mwezi uliopita, takriban watu 24 walikufa baada ya mito mashariki mwa Uganda kuvunja kingo zao.

Maeneo kadhaa ya Afrika Mashariki yamekumbwa na hali mbaya ya hewa mwaka huu, kupitia ukame wa muda mrefu na mvua nyingi zinasosababisha mafuriko. **BBC**



Baadhi ya raia wa kijiji cha Kasese, magharibi mwa Uganda chini ya milima ya Rwenzori wakijiokoa kwa kutumia matawi ya miti baada ya eneo hilo kukumbwa na mafuriko yaliyoambatana na maporomoko ya ardhi. **PICHA: AFP**

# UN yataka ukanda salama Zaporizhzhia

**NEWYORK,** MAREKANI

SHIRIKA la Kimataifa la Kudhibiti Nishati ya Atomiki (IAEA) limetoa wito wa kuwekwa ukanda salama karibu na kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia kinachodhibitiwa na Russia kilichokuwa kusini mwa Ukraine.

Kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia ambacho ni kikubwa zaidi barani Ulaya, kiliangukia mikononi mwa wanajeshi wa Russia mwezi Machi na kumekuwa na mashambulizi ya mara kwa mara karibu na eneo hilo, hali ambayo inazusha hofu ya kutokea janga la nyuklia.

limezihimiza Russia na Ukraine kuweka kile linachokiita Ukanda wa ulinzi na usalama wa Nyuklia karibu na kinu hicho.

Mkuu wa IAEA Rafael Grossi, alitoa onyo kali kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, siku chache baada ya kuongoza ujumbe wa ukaguzi katika kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia.

"Shambulizi lolote, iwe la kukusudia au kutokusudia, makombora ambayo kinu hiki kimepigwa, na hilo nilijionea binafsi na kutathmini, pamoja na watalaamu wangu, haikubaliki kabisa. Tunacheza na moto na jambo baya sana linaweza kutokea." alisema

Katika mkutano huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, aliwataka wanajeshi wa Russia na Ukraine kukubaliana kuhusu ukanda usiokuwa na shughuli za kijeshi.

Guterres alisema eneo la kinu halipaswi kuwa jukwaa la operesheni za kijeshi.

> **Guterres alisema eneo la kinu halipaswi kuwa jukwaa la operesheni za kijeshi.**

"Hiyo itajumuisha dhamira ya vikosi vya Russia kuwaondoa wanajeshi wote na vifaa kutoka kwenye ukanda huo na dhamira ya vikosi vya Ukraine kutoingia katika eneo hilo." alisema

Katika ripoti kuhusu ziara yake, IAEA ilisema mashambulizi ya makombora kwenye kinu hicho yanapaswa kusitishwa mara moja.

Ripoti hiyo ilisema hatua bora ya kuchukuliwa ni kusitishwa kwa vita, na kama hilo haliwezekani, basi eneo salama liwekwe.

**UKRAINE YASHAMBULIA MJI**

Vikosi vya Ukraine vilifanya mashambulizi katika mji wa Balaklia unaoshikiliwa na wanajeshi wa Russia ulioko mashariki katika jimbo la Kharkiv.

Hayo yalielezwa na ofisa mmoja mwandamizi wa kundi la wanaotaka kujitenga wanaoegemea upande wa Russia. Mashambulizi hayo yamefanyika katika wakati ambapo maofisa wa Ukraine wakiendelea kuwa na tahadhari kuhusu namna operesheni ya kukabiliana na mashambulizi ya Russia inavyokwenda.

Kwa mujibu wa gavana ´wa jimbo la Luhansk, Serhiy Gaidai, kuwa mashambulizi yanaendelea na vikosi vyao vinapata mafanikio ingawa hakufafanua maeneo yanakofanyika mashambulizi hayo.

Ilielezwa kwamba wanajeshi wa Ukraine wameshambulia maeneo 13 ya wanajeshi wa Russia kufikia jana asubuhi

**NAFAKA TOKA UKRAINE KUWASILI SOMALIA**

Wakati huo huo, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky amesema maelfu ya tani za nafaka kutoka nchini mwake zitawasili Somalia katika kipindi cha wiki chache zijazo.

Somalia inaelekea kukabiliwa na baa la njaa wakati mgogoro wa kidunia wa usalama wa chakula na mabadiliko ya tabia nchi yakiwa ni mambo yanayohatarisha maisha ya mamilioni ya watu.

Rais Zelensky alitoa tamko lake baada ya Rais wa Urusi Vladmir Putin, kuzishutumu nchi za magharibi kwa kupeleka barani ulaya shehena nyingi za nafaka kutoka bandari za Ukraine badala ya nchi masikini na sehemu zinazokabiliwa na njaa zaidi duniani.

Rais Putin akizungumza katika jukwaa la kiuchumi katika mji wa Vladivostock, alizishutuhumu nchi za magharibi kwa kuendesha vitendo vya kikoloni na kusema kwamba nchi yake huenda ikazungumza na Uturuki kuhusu kuyatathimini upya makubaliano yaliyoifanya nchi yake kuondoa vizuizi vyake katika bandari za Ukraine na kuziruhusu meli kutumia njia hiyo.

Russia ilishawahi kutoa madai hayo hapo awali lakini, kauli ya kiongozi huyo ni ya kwanza kuyataja mataifa hayo.

**DW**

# GEITA, KAGERA USHINDI MGUMU LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

SARE ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba juzi kati ya wenyeji Geita Gold na Kagera Sugar, imezifanya timu hizo kutopata ushindi wowote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara tangu ianze ikiwa imeingia raundi ya tatu.

Mabao ya Abeid Athumani wa Kagera Sugar dakika ya 43 na la kusawazisha la Selemani Ibrahim wa Geita Gold, limezifanya timu hizo 'kubaniana' kupata ushindi wa kwanza kwenye Ligi Kuu.

Kwenye mechi ya kwanza Geita Gold ilichapwa mabao 3-0 dhidi ya Simba, na baadaye kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Azam FC.

Kagera Sugar nayo iliingia uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Azam FC na mechi ya pili 2-0 dhidi ya Simba.

Kocha Mkuu Francis Baraza, alisema hali ya hewa ya Mwanza iliwaathiri kwa sababu ni tofauti sana na ya Bukoba mkoani Kagera, akiongeza kuwa makosa madogo waliyoyafanya wachezaji wake yalisababisha wenyeji warudishe bao.

"Mechi ilikuwa kwa timu zote mbili, Geita walikuwa nyumbani walijituma zaidi, watoto wangu walifanya makosa wenyeji wakasawazisha, hali ya hewa ya Mwanza nayo ni tofauti na Bukoba ilituathiri pia, lakini nawapongeza vijana wangu kwa sababu tumecheza mechi zote tatu ugenini, tunafanya kila njia kuanza kupata matokeo ugenini," alisema Baraza.

Kocha Msaidizi wa Geita Gold, Mathias Wandiba, naye alikiri ugumu wa mechi hasa kutokana na timu zote mbili kutoshinda michezo ya raundi mbili za mwanzo.

"Mechi ilikuwa ngumu, kila mtu alihitaji matokeo, kila timu kwenye mechi kabla ya hii ilikuwa haijapata matokeo kwa hiyo kila moja ilijitahidi kutaka kupata ushindi kwa mwenzake, lakini haikuwezekana," alisema.

Geita Gold ina pointi mbili kwenye mechi tatu ilizocheza, huku Kagera Sugar ikiwa na pointi moja.

## CHUKUA HIYO...



Mchezaji wa Tenis, Bakari Kiando, akipiga mpira kuurudisha kwa mpinzani wake wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Ghmkhana jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Namungo yarejea Uwanja wa Majaliwa

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Namungo imerejea kwenye uwanja wake wa nyumbani, Majaliwa uliopo Ruangwa mkoani Lindi baada ya kutoutumia kwa msimu mzima kutokana na kuwa katika matengenezo.

Kikosi hicho kiliwasili juzi jioni kikitokea jijini Dar es Salaam kilipokuwa kimeweka kambi na kupokelewa na mamia ya mashabiki wa timu hiyo wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Hassan Ngoma.

Akizungumza kwenye mapokezi hayo, Mkuu huyo wa wilaya, alisema mapokezi hayo yamekuwa ni deni kwa wachezaji wa timu hiyo.

"Wachezaji wetu mmewapa deni, wanafahamu kuwa mnayo shauku na kiu ya mabao, mnataka kuona timu inamaliza nafasi tatu za juu," alisema Ngoma akishangiliwa na mashabiki waliojitokeza.

Nahodha wa timu hiyo, Jacob Massawe, akizungumza kwa niaba ya wachezaji, alielezea furaha waliyonayo kurejea tena kwenye uwanja wa nyumbani. "Tuna furaha sana, siyo sisi tu wachezaji bali hata mashabiki wetu walitamani sana kutuona, matarajio yao makubwa ni kuona tunafanya vizuri," alisema Massawe.

Meneja wa timu hiyo, Idrisa Bandari, alisema msimu huu malengo yao ni kuwa kwenye nafasi tatu za juu, na wanataka kushinda mechi si za nyumbani tu, bali hata ugenini.

Kwa msimu mzima, Uwanja wa Majaliwa ulikuwa kwenye matengenezo makubwa, pamoja na mambo mengine, umewekwa nyasi bandia na taa kwa mechi za usiku.

Msimu uliopita, timu hiyo ilicheza mechi zake kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, huku msimu huu ikianza kucheza mechi yake ya nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mpaka dhidi ya Mtibwa Sugar na kutoka sare ya mabao 2-2.

## Mfaransa wa Azam FC akunwa na vipaji

**Na Hadija Mngwai**

UONGOZI wa Azam FC, umesema kocha mpya wa timu hiyo, Mfaransa Denis Lavagne, ameeleza kukunwa na ubora wa kikosi cha timu hiyo baada ya kukiangalia kikimenyana dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Lavagne ambaye ametua kuchukua mikoba ya Abdihamid Moallin, aliishuhudia Azam ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya mabingwa watetezi, Yanga juzi.

Akizungumza na Nipashe jana lilipotaka kujua tathimini ya Lavagne baada ya kuiona kwa mara ya kwanza timu hiyo, Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema Mfaransa huyo amekisifia kikosi chake na kueleza kinahitaji maboresho madogo tu kuwa fiti zaidi.

"Mwalimu amekiangalia kikosi, amesema wachezaji wote ni bora na wanavipaji, kikosi kipo vizuri kinahitaji maboresho kidogo. Baada ya mechi kuisha amekwenda kuwasalimia wachezaji kwa mara ya kwanza na amewapongeza na kusema kuna vitu vichache ambavyo vinahitaji kufanyiwa marekebisho ili timu iwe nzuri," alisema Popaty.

## Wasanii kibao kutoa burudani Fiesta 2022

**Na Sabato Kasika**

WASANII kibao wa muziki wa kizazi kipya wanatarajiwa kutoa burudani katika onyesho la kwanza la msimu wa Fiesta 2022, litakalofanyika Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga mkoani Rukwa mwezi huu.

Baadhi ya wasanii watakaokuwapo katika Fiesta ya mwaka huu ni Ali Kiba, Abdul Kiba, Juma Jux, Rayvanny, Marioo, Sarafina, Kundi la Weusi, Kussa, Mr. Blue, Coutry Boy, Maarifa, Stamina, Kayumba, Nay wa Mitego, Jay Melody, Young Lunya, Dogo Janja na Dulla Makabila.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya msimu wa Fiesta 2022, Sebastian Maganga, jijini Dar es Salaam juzi, katika uzinduzi wa mwaka mpya na tukio hilo la burudani ambalo sasa linatimiza miaka 18.

Katika uzinduzi huo wasanii waliopanda jukwaani lililotengenezwa kwa ubunifu wa kutumia makontena, walitoa fursa kwa ndugu, marafiki, wadau wa burudani na wafanyakazi wa Clouds kukusanya maoni ya jinsi ya kufanikisha Fiesta ya mwaka huu.

"Sababu ya kuzindua msimu juu ya kontena, ni ishara ya utajiri mkubwa na zawadi kwa wasanii, na kwenye mipango yetu tunatarajia kumwomba Anko Tajiri kuwa sehemu ya Fiesta 2022, na uzuri makontena yamefunguka kuashiria kuanza kwa msimu wa Fiesta 2022," alisema Maganga.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CARROLL ATAKIWA WOLVES**
KLABU ya Wolves itaelekeza nguvu zake kumnasa mshambuliaji wa zamani wa England, Andy Carroll mwenye umri wa miaka 33 ambaye yuko huru kama watashindwa kumsajili, Diego Costa. ***(Telegraph)***

**DE JONG AWINDWA CHELSEA**
MANCHESTER United na Chelsea zitaendelea kufuatilia mustakabali wa kiungo wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, pale Barcelona kabla ya kujaribu kumnasa Januari. ***(Caught Offsice)***

**LUIZ KUONDOKA VILLA**
KIUNGO wa Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 24, anajiandaa kuondoka Aston Villa kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu. ***(UOL)***

**REDMOND KUTUA BESIKTAS**
WINGA wa Southampton, Nathan Redmond mwenye umri wa miaka 28, anatarajiwa kujiunga na Besiktas ya Uturuki kwa mkataba wa mwaka mmoja. ***(Fabrizio Romano)***

**MENDY AIGOMEA CHELSEA**
GOLIKIPA wa Chelsea na Senegal, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 30, amekataa ofa ya kwanza ya kusaini mkataba mpya kwa sababu ya mshahara mdogo uliowekwa ambao ni mdogo kuliko anaopata mlinda mlango namba mbili wa timu hiyo, Kepa Arrizabalaga. ***(Standard)***

**SALIHAMIDZIC NA KANE**
MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amepuuzilia mbali tetesi zinazoihusisha klabu hiyo na mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29. ***(talkSPORT)***

**BROBBEY NA TEN HAG**
MSHAMBULIAJI wa Ajax, Mholanzi Brian Brobbey mwenye umri wa miaka 20, amesema alitafutwa na kocha Erik ten Hag ili ajiunge na Manchester United msimu huu. ***(ESPN.nl via Voetbal Primeur)***

**ALZATE KWENDA STANDARD**
KIUNGO wa Brighton na Colombia, Steven Alzate mwenye umri wa miaka 23, yuko kwenye mazungumzo na Standard Liege ya kujiunga nayo kwa mkopo wa mpaka mwishoni mwa msimu. ***(Telegraph)***

**NICOLO MKATABA MPYA**
AS Roma inataka kumpa mkataba mpya kiungo majeruhi wa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL ATIMULIWA CHELSEA

●●● Nilikuwa kwenye sinema isiyo sahihi, nina hasira na uchezaji wetu...

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel amefutwa kazi kutokana na mwendelezo mbaya wa matokeo unaoikabili timu hiyo.

Kufukuzwa kwake kumekuja saa chache baada ya kupokea kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Dinamo Zagreb kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne usiku.

'The Blues' sasa wamepoteza mechi tatu mfululizo za ugenini kwa mara ya kwanza chini ya Tuchel, wakiwa na mwenendo mbaya zaidi ugenini tangu Desemba 2020 chini ya Frank Lampard.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Klabu hiyo, wamefikia makubaliano ya pande zote mbili kuvunja mkataba wake.

Baada ya mchezo wa juzi, Tauchel alinukuliwa akiwalalamikia wachezaji kutokuwa na njaa ya kutafuta mabao.

"Sikuona chochote, ni wazi nilikuwa kwenye sinema isiyo sahihi," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Nilifikiri kwamba mchezo uliopita ulitusaidia. Nilidhani timu ilikuwa imejiandaa, nilifikiri tulijua hii inahusu nini.

"Sijui kwa hakika utendaji huu wa leo (juzi) unatoka wapi. Ukosefu wa dhamira, ukosefu wa njaa na ukosefu wa nguvu ya kufanya mambo ambayo tunahitaji kwa kiwango cha juu.

"Ni wazi hatuko tunakotaka kuwa. Nina hasira na uchezaji wetu.

"Si sahihi vya kutosha, si mkali vya kutosha kwenye mpira, haijaamuliwa vya kutosha. Haifai mtu mmoja, haitoshi kama timu."

Tuchel alijiunga na timu hiyo mwaka 2021 ambapo alifanikiwa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka huohuo.

Kocha huyu ameondoka akiwa amecheza michezo sita kwenye Ligi Kuu England (EPL), msimu huu huku akishinda mechi tatu, sare moja na kupoteza michezo miwili.

Ameiacha timu hiyo ikiwa nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,029,4


JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 08 NA 09 SEPTEMBA 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.08/09/22 | 19:45 | Slovacko vs Partizan | 2.73 | 3.34 | 2.48 |
| 02.08/09/22 | 19:45 | Nice vs FC Koln | 2.50 | 3.32 | 2.71 |
| 03.08/09/22 | 22:00 | Ferencvaros TC vs Trabzonspor | 2.38 | 3.24 | 2.93 |
| 04.08/09/22 | 22:00 | Sturm Graz vs Midtjylland | 2.62 | 3.27 | 2.62 |
| 05.08/09/22 | 22:00 | Nantes vs Olympiakos | 2.32 | 3.29 | 2.99 |
| 06.09/09/22 | 01:00 | Criciuma SC vs Bahia BA | 2.70 | 2.84 | 2.65 |
| 07.09/09/22 | 19:00 | EN Paralimni vs Doxa Katokopia | 2.57 | 3.07 | 2.82 |
| 08.09/09/22 | 20:00 | Sochi vs Dinamo Moscow | 2.24 | 3.55 | 2.85 |
| 09.09/09/22 | 20:00 | Oliveirense vs Penafiel | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 10.09/09/22 | 20:30 | FC Versailles 78 vs Dunkerque | 2.53 | 2.98 | 2.83 |
| 11.09/09/22 | 20:30 | Sedan vs Avranches | 2.68 | 3.23 | 2.48 |
| 12.09/09/22 | 20:30 | Cholet vs Orleans | 2.75 | 3.20 | 2.45 |
| 13.09/09/22 | 21:45 | Shelbourne vs Sligo Rovers | 2.43 | 2.95 | 2.86 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa · vodacom m-pesa · airtel money · ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BAYERN YAKANUSHA KUMWINDA HARRY



**MUNICH, Ujerumani**

MKURUGENZI wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amesisitiza kuwa klabu hiyo haifanyi chochote nyuma ya pazia ili kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane msimu ujao wa majira ya joto.

Miamba hao wa Bundesliga walionyesha waziwazi kumtaka Kane msimu huu wa majira ya joto, jambo ambalo lilimkasirisha kocha Antonio Conte, na ripoti nchini Ujerumani zimedai kuwa wanajaribu kumshawishi mshambuliaji huyo kukataa ofa ya Tottenham ya kumpa mkataba mpya.

Mkataba wa Kane unamalizika mwaka 2024 na kwa mujibu wa ripoti, Bayern wanaamini wangeweza kumsajili mwaka 2023 ikiwa amebakiza mwaka mmoja tu.

Na Salihamidzic alisema Jumanne kwamba, wao kama Bayern Munich hawana mpango huo.

"Sidhani Oliver Kahn (Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Bayern) anashinikiza kumsajili (Kane)," alisema akinukuliwa na Bild.


"Nyote mnaweza kuchukua hatua nyuma huko, hakuna chochote juu yake."

90min inaelewa kuwa Kane na Tottenham wana nia ya pande zote kujadili mkataba mpya, ingawa hakuna upande wowote ambao uko katika haraka ya kufungua mazungumzo.

Kane anasemekana kuwa na furaha na maisha chini ya Conte na alifurahishwa na kocha huyo alivyofanya soko la uhamisho wa majira ya joto, ambapo fedha nyingi zilitumika kuwasajili Richarlison, Cristian Romero, Yves Bissouma, Destiny Udogie, Djed Spence, Ivan Perisic na Fraser Forster.

# Man City yajipanga kumnasa Kroos

**MANCHESTER, England**



MANCHESTER City wanapanga kusajili kiungo wa kati wa Real Madrid, Toni Kroos katika dirisha la Januari, kwa mujibu wa El Nacional.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England, Manchester City wanaweza kuwa tayari kufanya biashara hiyo Januari.

Kikosi hicho cha Kocha Pep Guardiola kiliwaongeza Erling Haaland, Kalvin Phillips, Sergio Gomez na Manuel Akanji katika dirisha la uhamisho lililopita.

Lakini City huenda wanataka kuimarisha zaidi kikosi chao huku kukiwa na mkanganyiko wa ratiba msimu wa 2022-23.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekataa ofa ya Madrid ya kuongeza muda.

KANE.JPG

'Los Blancos' wanaweza kufikiria kumuuza Kroos Januari na Guardiola ni mtu anayevutiwa naye kwa muda mrefu.

HABARI MICHEZO

# 401,974/-

# VIGOGO WA SOKA KDFA WATIMULIWA KWA UBADHIRIFU

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKUTANO Mkuu wa dharura wa Chama cha Soka Wilaya ya Kahama (KDFA), umewafukuza kazi viongozi watatu wa chama hicho baada ya kubainika na makosa mbalimbali ikiwamo matumizi mabaya ya ofisi na kukisababishia hasara ya zaidi ya Sh. milioni nne.

Waliofukuzwa uongozi ni pamoja na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa KDFA Wilaya, Okuku Obata, Katibu Mtendaji, Fadhili Kipindula na Mwakilishi wa Klabu, Donald Igulu.

Maamuzi hayo yalifanyika katika mkutano mkuu wa dharura wa chama hicho, uliofanyika jana chini ya usimamizi wa Chama cha Soka Mkoa wa Shinyanga (SHIREFA), huku ajenda kuu ya ikiwa ni kujadili mapato na matumizi ya KDF ambayo yamekuwa yakipatikana kwenye Ligi Daraja la Kwanza inayoendelea.

Uamuzi huo ulifikiwa na wajumbe wa mkutano huo baada ya viongozi hao kubainika na tuhuma za ubadhirifu wa fedha za KDFA, matumizi mabaya ya nyaraka za ofisi kwa kutembea nazo kwenye mabegi yao na pia kuwatenga wajumbe wengine wa kamati tendaji kinyume cha katiba ya chama hicho.

Aidha, wajumbe wa mkutano huo walikaa na kupiga kura za siri kwa mujibu wa katiba ya chama hicho kati ya wajumbe 59 kura 57 zilifikia maamuzi ya kuwafukuza na kuvua madaraka ndani ya chama na kutakiwa kurejesha fedha zilizopotea ndani ya uongozi wao.

Hata hivyo, mkutano huo umeiagiza kamati tendaji inayoongozwa na Kaimu Mwenyekiti wa KDFA, Hamis Shilinde, kuhakikisha ndani ya siku 30 uchaguzi unafanyika kuziba nafasi zilizowazi ambazo ni Mwenyekiti wa KDFA, makamu mwenyekiti, katibu mkuu, mjumbe wa klabu na mjumbe wa mkutano mkuu nafasi iliyokuwa wazi.

Awali akijitetea mbele ya wajumbe wa mkutano huo aliyekuwa Mwenyekiti wa KDFA, Obata, alikanusha kutumia vibaya fedha za chama hicho kutokana na yeye kutohusika katika ukusanyaji wa maduhuli ya chama hicho.

"Fedha zinazoingia KDFA zilikuwa zinakusanywa na katibu wangu na mimi sijui chochote juu fedha hizi, niliamini zinapopatika zinapelekwa benki kama katiba ya chama inayoelekeza na si vingine,"alisema Obata.

Kwa upande wa Katibu wa SHIREFA, Michael Kaijege, alisema wao wanaheshimu maamuzi ya mkutano huo mkuu na wanasubiri vikao vya mkoa ili kufanya maamuzi ya pamoja ya namna ya kuendelea kuchukua hatua za kisheria.

**KIDIGITALI...**



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Boompay, Natasha Stambuli (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza kuimarisha huduma ya kusikiliza muziki kidigitali kupitia App yao baada ya kujiunga na vifurushi vya tiGO. Katikati ni Meneja wa Chapa wa tiGO, William Mpinga na kulia ni balozi wa huduma hiyo msanii wa muziki wa kizazi kipya, Omary Ali maarufu Marioo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kipanga yawafuata Wasudani CAF Dar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAWAKILISHI wa Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Maafande wa Kipanga, wanatarajia kuwasili Dar es Salaam leo tayari kwa mchezo wao wa awali wa michuano hiyo dhidi ya Hilal FC Wau ya Sudan ya Kusini.

Kipanga itacheza mchezo wake wa ugenini Jumapili wiki katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam majira ya saa 10 alasiri.

Timu ya Kipanga inatarajiwa kusafiri na msafara wa watu 30 wakiwamo wachezaji pamoja na viongozi wa timu hiyo. Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Khamis Hassan, alisema timu yake imejiandaa vizuri kuhakikisha inapata matokeo mazuri katika mchezo huo wa ugenini.

Alisema anajua mchezo wa ugenini utakuwa mgumu kwao, lakini wamejiandaa kuhakikisha wanasonga mbele katika michuano hiyo.

"Wachezaji wetu mpaka sasa wapo vizuri wote ambao tumewasajili kwa ajili ya michuano ya kimataifa wapo vizuri na wanaendelea na maandalizi ya mwisho mwisho kuelekea mchezo huo muhimu,"alisema.

Kipanga ipo chini ya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) ambapo mchezo wao wa nyumbani utapigwa Uwanja wa Amaan, Zanzibar Septemba 16, mwaka huu.

Hilal FC Wau imeomba kuutumia Uwanja wa Azam Complex kama wao wa nyumbani kutokana na hali ya machafuko nchini kwao, Sudan Kusini.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 10/09/22 | 17:00 | KV Kortrijk vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.46 | 3.45 | 2.60 |
| 02. 10/09/22 | 17:00 | Shrewsbury Town vs Oxford United | 2.50 | 3.25 | 2.65 |
| 03. 10/09/22 | 17:00 | Birmingham City vs Swansea City | 2.80 | 3.15 | 2.46 |
| 04. 10/09/22 | 17:00 | Barnsley vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.48 |
| 05. 10/09/22 | 17:00 | Southampton FC vs Brentford FC | 2.34 | 3.35 | 2.80 |
| 06. 10/09/22 | 17:00 | Leicester City vs Aston Villa | 2.45 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 10/09/22 | 17:15 | Espanyol Barcelona vs Sevilla FC | 2.90 | 3.10 | 2.41 |
| 08. 11/09/22 | 14:30 | KVC Westerlo vs RSC Anderlecht | 2.75 | 3.35 | 2.38 |
| 09. 11/09/22 | 16:00 | West Ham United vs Newcastle United | 2.37 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 11/09/22 | 16:00 | Sassuolo Calcio vs Udinese Calcio | 2.60 | 3.40 | 2.48 |
| 11. 11/09/22 | 16:00 | Angers SCO vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 11/09/22 | 16:00 | Leixoes SC vs SC Farense | 3.00 | 3.15 | 2.33 |
| 13. 11/09/22 | 16:30 | 1. FC Cologne vs Union Berlin | 2.48 | 3.30 | 2.65 |
| 14. 11/09/22 | 17:15 | Spal Ferrara vs Venezia FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 15. 11/09/22 | 17:30 | FC Pacos Ferreira vs Casa Pia Lisbon | 2.70 | 3.00 | 2.65 |
| 16. 11/09/22 | 21:45 | AS Monaco vs Olympique Lyon | 2.50 | 3.40 | 2.60 |
| 17. 11/09/22 | 22:00 | Real Betis Seville vs Villarreal CF | 2.60 | 3.25 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 08/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2691 | Shirak Gyumri vs Van Yerevan | 2.54 | 2.88 | 2.78 |
| 16:00 | 1488 | CA Lanus vs CA Barracas Central Reserve | 1.54 | 3.92 | 5.10 |
| 16:00 | 3843 | Mukura vs AS Kigali | 3.14 | 2.80 | 2.36 |
| 16:00 | 4075 | Bugesera FC vs APR FC | 6.50 | 3.35 | 1.55 |
| 16:30 | 4220 | Bunyodkor vs Neftchi Fargona | 1.62 | 3.72 | 4.70 |
| 17:00 | 2475 | Defensa Y Justicia Reserve vs CA Talleres de Cordoba Reserve | 2.00 | 3.24 | 3.43 |
| 17:00 | 3192 | CA Platense vs Patronato Reserve | 2.05 | 3.15 | 3.40 |
| 17:00 | 5124 | Colon de Santa Fe Reserve vs Banfield Reserve | 2.60 | 3.09 | 2.55 |
| 17:30 | 3484 | Qizilqum vs FC Olimpik | 1.98 | 3.04 | 3.77 |
| 18:00 | 2948 | FK Silas vs FK Atmosphere | 1.67 | 3.93 | 4.03 |
| 18:00 | 3405 | Khalijfars Mahshahr vs Khosheh Talaei | 3.04 | 2.79 | 2.42 |
| 19:00 | 1012 | Moghayer AL Sarhan vs Sahab Club | 3.38 | 2.94 | 2.16 |
| 19:00 | 2107 | Otterup B & IK vs BK Marienlyst | 5.09 | 4.90 | 1.43 |
| 19:00 | 2668 | Police FC Rwanda vs Rayon Sports FC | 2.55 | 2.80 | 2.85 |
| 19:00 | 3137 | Al Nahda (Oman) vs Sohar Club | 1.73 | 3.30 | 5.00 |
| 19:30 | 5231 | Sola vs Brodd | 4.31 | 4.02 | 1.62 |
| 19:45 | 1255 | Union Berlin vs Union Saint Gilloise | 1.55 | 4.27 | 5.29 |
| 19:45 | 1868 | HJK Helsinki vs Betis | 8.09 | 5.06 | 1.34 |
| 19:45 | 1956 | Fiorentina vs Rigas Futbola Skola | 1.12 | 7.87 | 20.17 |
| 19:45 | 2236 | Malmo vs Sporting Braga | 3.18 | 3.38 | 2.17 |
| 19:45 | 2398 | FC Zurich vs Arsenal | 8.02 | 5.03 | 1.34 |
| 19:45 | 2423 | Hearts vs Basaksehir | 3.13 | 3.28 | 2.24 |
| 19:45 | 2479 | Fenerbahce vs Dynamo Kiev | 1.65 | 3.89 | 4.85 |
| 19:45 | 3274 | Villarreal vs Lech Poznan | 1.24 | 6.05 | 10.09 |
| 19:45 | 3485 | Ludogorets Razgrad vs Roma | 5.65 | 4.23 | 1.52 |
| 19:45 | 3730 | AEK Larnaca vs Rennes | 4.85 | 3.84 | 1.66 |
| 19:45 | 3845 | PSV Eindhoven vs Bodo Glimt | 1.38 | 5.05 | 6.67 |
| 19:45 | 4460 | Nice vs FC Koln | 2.50 | 3.32 | 2.71 |
| 19:45 | 4542 | Slovacko vs Partizan | 2.56 | 3.37 | 2.61 |
| 19:45 | 4581 | Austria Vienna vs Hapoel Beer Sheva | 2.10 | 3.44 | 3.29 |
| 19:45 | 4692 | KF Ballkani vs CFR Cluj | 3.30 | 3.30 | 2.20 |
| 19:45 | 5685 | Anderlecht vs Silkeborg | 1.64 | 3.89 | 4.95 |
| 21:00 | 4112 | Al Shabab Riyadh vs AL Tai | 1.33 | 5.24 | 7.86 |
| 22:00 | 1358 | FC Basel vs Pyunik Yerevan | 1.15 | 7.29 | 15.18 |
| 22:00 | 1476 | Sivasspor vs Slavia Prague | 3.47 | 3.37 | 2.10 |
| 22:00 | 1541 | Ferencvaros TC vs Trabzonspor | 2.32 | 3.28 | 2.98 |
| 22:00 | 1576 | Nantes vs Olympiakos | 2.35 | 3.32 | 2.92 |
| 22:00 | 1624 | Slovan Bratislava vs Zalgiris | 1.72 | 3.58 | 4.74 |
| 22:00 | 2374 | Omonia Nicosia vs Sheriff Tiraspol | 2.25 | 3.13 | 3.28 |
| 22:00 | 2599 | SC Freiburg vs Karabakh | 1.39 | 4.75 | 7.07 |
| 22:00 | 3076 | SC Dnipro 1 vs AZ Alkmaar | 5.46 | 4.15 | 1.55 |
| 22:00 | 4060 | Lazio vs Feyenoord | 2.01 | 3.59 | 3.39 |
| 22:00 | 4327 | Red Star Belgrade vs Monaco | 3.17 | 3.52 | 2.12 |
| 22:00 | 4525 | West Ham vs Steaua Bucuresti | 1.20 | 6.25 | 13.10 |
| 22:00 | 4817 | Manchester Utd vs Real Sociedad | 1.67 | 3.69 | 4.98 |
| 22:00 | 5326 | FC Vaduz vs Apollon Limassol | 3.12 | 3.37 | 2.21 |
| 22:00 | 5357 | Sturm Graz vs Midtjylland | 2.62 | 3.27 | 2.62 |
| 22:00 | 5837 | Molde vs KAA Gent | 2.01 | 3.66 | 3.33 |
| 22:00 | 5997 | Shamrock Rovers vs Djurgardens IF | 3.37 | 3.43 | 2.08 |
| 22:30 | 2470 | Santiago Morning vs Deportes Recoleta | 2.19 | 3.09 | 3.14 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Septemba 8, 2022
Nipashe

UKURASA 21



## Tuchel atimuliwa Chelsea

# Nabi aanika sababu Azam kuishika Yanga

### Amtaja Mwamnyeto, Job huku akilia na safu ya ushambuliaji kukosa...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushindwa kuendeleza kasi yao ya ushindi kwenye Ligi Kuu Bara mbele ya Azam FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameanika kinachokitesa kikosi chake huku akitaja muunganiko hususan katika safu ya ushambuliaji bado ni tatizo jambo ambalo anaendelea kulifanyia kazi.

Katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2, ilikuwa ya kasi kwa dakika zote 90 huku Yanga ikitokea nyuma kwa mabao yote mawili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema mechi ilikuwa ngumu kwa sababu pande zote mbili zilijiandaa vizuri, na Azam ni timu nzuri na ilikuwa vizuri na bora katika mipira iliyokufa, hivyo kufanikiwa kupata mabao mawili.

Alisema kwa Yanga hawakuwa na muunganiko mzuri jambo ambalo lilichangia kushindwa kuzibadili nafasi nyingi walizotengeneza kuwa mabao.

"Kutotumia nafasi hizo ndicho kilisababisha mchezo huu wa leo kuonekana mgumu sana na kuwa na ushindani mkubwa, tumeona makosa katika safu ya ulinzi, huwezi kusema ya wachezaji wawili Mwamnyeto (Bakari) na Job (Dickson), bali ni makosa ya timu nzima kwa sababu ukabaji wetu haukuwa nzuri.

"Tungekuwa na ukabaji mzuri ile mipira ya kufa waliyopata Azam FC tusingefungwa kabisa, Job hakucheza nafasi yake na alibeba majukumu Shaban (Djuma) alikuwa anaumwa," alisema Nabi ambaye hata hivyo alilazimika kumwingiza Djuma kipindi cha pili.

Alisema Kibwana (Shomari) ana matatizo na yalionekana kwenye mchezo wa Timu ya Taifa (Stars), kwenye mpira huwezi kumlaumu mchezaji mmoja bali makosa yanabebwa na timu nzima.

"Niliiona Azam FC katika michezo yao ya kirafiki na kubaini ubora wao na kabla ya mechi nilisema mechi itakuwa na ushindani mkubwa".

Kuhusu rafu ya Bernard Morrison ya kumkanyaga tumboni Sospeter Bajana, Nabi alimtetea kwa kusema: Morrison ni mchezaji mwenye nidhamu kwa sababu anaheshimu kila mtu licha ya muda mwingi kufanya vichekesho".

Wakati Nabi akisema hayo, Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kali Ongala, alisema kipindi cha kwanza walicheza vizuri na kutengeneza nafasi nyingi, lakini washindwa kuzitumia kwa kukosa utulivu katika safu ya ushambuliaji.

"Tumekosa pointi tatu, lakini moja tunashukuru na tumemalizana na Yanga, sasa tunaenda Mbeya dhidi ya Mbeya City na kuendelea kutafuta pointi katika michezo ijayo.

"Tumeona madhaifu yetu na tunarejea uwanjani kuyafanyia kazi...safu ya ushambuliaji bado nina wachezaji wenye vipaji, sitachoka kwa sababu tunatengeneza nafasi nyingi, hivyo ninaimani tutafanikiwa kwa hilo," alisema Kali.

**KAZI KAZI...**



Mshambuliaji wa Azam FC, Kipre Junior, akimtoka beki wa Yanga, Yannick Bangala, wakati timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi usiku. **MPIGAPICHA WETU**



## Namungo yarejea Uwanja wa Majaliwa

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Namungo imerejea kwenye uwanja wake wa nyumbani, Majaliwa uliopo Ruangwa mkoani Lindi baada ya kutoutumia kwa msimu mzima kutokana na kuwa katika matengenezo.

Kikosi hicho kiliwasili juzi jioni kikitokea jijini Dar es Salaam kilipokuwa kimeweka kambi na kupokelewa na mamia ya mashabiki wa timu hiyo wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Hassan Ngoma.

UK. 20

## Kipanga yawafuata Wasudani CAF Dar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**



WAWAKILISHI wa Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Maafande wa Kipanga, wanatarajia kuwasili Dar es Salaam leo tayari kwa mchezo wao wa awali wa michuano hiyo dhidi ya Hilal FC Wau ya Sudan ya Kusini.

Kipanga itacheza mchezo wake wa ugenini Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam majira ya saa 10 alasiri.

UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >